JAMHURI YA MUUNGANO



# TAARIFA YA MIAKA 50 YA UHURU WA TANZANIA BARA (1961 - 2011)

MIAKA HAMSINI YA UHURU TANZANIA BARA

1961 - 2011

TUMETHUBUTU, TUMEWEZA TUNAZIDI KUSONGA MBELE



...amhuri ya Muungano ... akikagua gwaride la askari wa Jeshi la Polisi

# TAARIFA YA MIAKA 50 YA UHURU WA TANZANIA BARA

# (1961 – 2011)

# YALIYOMO


YALIYOMO ........ i

Ujumbe wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ........ iv

Ujumbe wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ....... v

HISTORIA YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI ........ 1

Jeshi la Polisi wakati wa Utawala wa Kijerumani 1886-1919 ........ 1

Jeshi la Polisi wakati wa utawala wa Waingereza 1919-1961 ........ 2

Jeshi la Polisi kuanzia mwaka 1961 ........ 4

Jeshi la Polisi mwaka 1964 ........ 4

Jeshi la Magereza wakati wa ukoloni ........ 5

Mafunzo ya Watumishi Wakati wa Ukoloni ........ 5

Jeshi la Magereza Baada ya Uhuru ........ 6

Utawala na Uendeshaji wa Magereza ........ 7

Muundo na Majukumu ya Jeshi la Magereza ........ 8

Uongozi katika Ngazi ya Mikoa ........ 8

Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ........ 9

Idara yaUhamiaji ........ 10

Majukumu ya Idara ya Uhamiaji baada ya Uhuru ........ 11

Majukumu ya Idara ya Uhamiaji baada ya Muungano ........ 12

Idara ya Wakimbizi ........ 13

Hifadhi ya wakimbizi kwenye Makazi 1960 - 1980 ........ 14

Idara ya Huduma kwa Jamii .......... 18
Idara ya Malalamiko .......... 19
Idara ya Huduma za Sheria .......... 19
Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa .......... 20
MUUNDO WA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI .......... 22
Kuanzishwa kwa Wizara ya Usalama wa Raia .......... 22
Muundo wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi (Chati) .......... 24
MAJUKUMU YA WIZARA .......... 25
Jeshi la Polisi .......... 25
Jeshi la Magereza .......... 26
Jeshi la Zimamoto na Uokoaji .......... 26
Idara ya Uhamiaji .......... 26
Idara ya Wakimbizi .......... 26
Huduma kwa Jamii .......... 27
Idara ya Kushughulikia Malalamiko .......... 28
Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa .......... 28
HALI YA UONGOZI KUANZIA 1961 .......... 29
MAFANIKIO YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI .......... 32
Jeshi la Polisi .......... 33
Jeshi la Magereza .......... 40
Jeshi la Zimamoto na Uokoaji .......... 49
Idara ya Uhamiaji. .......... 50
Idara ya Wakimbizi .......... 52
Idara ya Huduma kwa Jamii .......... 53
Idara ya Malalamiko .......... 55

Idara ya Huduma za Sheria ........ 55

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ........ 55

CHANGAMOTO ZA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI ........ 57

Jeshi la Polisi ........ 57

Jeshi la Magereza ........ 58

Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ........ 59

Idara ya Uhamiaji ........ 59

Idara ya Wakimbizi ........ 60

Idara ya Huduma kwa Jamii ........ 60

Idara ya Kushughulikia Malalamiko ........ 60

Idara ya Huduma za Sheria ........ 61

Mamlaka ya Vitambulisho ya Taifa ........ 62

MATARAJIO YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 50 IJAYO ........ 62

HITIMISHO ........ 63



## Ujumbe wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi

*Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi,* ***Mhe. Shamsi Vuai Nahodha***

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina jukumu la kulinda usalama wa raia na mali zao, kuhifadhi na kuwarekebisha wafungwa, kudhibiti uingiaji na utokaji nchini wa raia na wageni, kutoa huduma za zimamoto na uokoaji, kuwahudumia wakimbizi waliopo nchini, kutekeleza programu ya Huduma kwa Jamii na kutoa vitambulisho vya Taifa. Majukumu haya yanatekelezwa kupitia Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Idara ya Wakimbizi na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

Tukiwa tunaadhimisha Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara, nchi yetu inaendelea kuwa na amani na utulivu. Kutokana na hali hii, nchi yetu imeweza kupata maendeleo makubwa katika sekta za kiuchumi na kijamii. Ili kuimarisha amani na utulivu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na vitendo vya uhalifu ili kulinda usalama wa raia na mali zao. Katika kufikia azma hii, Wizara kwa kupitia Jeshi la Polisi imebuni dhana ya Polisi Jamii au Ulinzi Shirikishi. Hivi sasa Jeshi la Polisi linashirikiana na wananchi kuwabaini wahalifu ili kuwachukulia hatua za kisheria.

Dhana ya Polisi Jamii inatekelezwa katika maeneo mbalimbali ya nchi na Jeshi la Polisi litaendelea kuwashirikisha wananchi katika shughuli za ulinzi na usalama. Iwapo wananchi watashiriki kikamilifu katika shughuli za ulinzi na usalama, hapana shaka nchi yetu itapiga hatua kubwa za maendeleo.

**Tumethubutu, tumeweza tunazidi kusonga mbele.**

Shamsi Vuai Nahodha (Mb),
**Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.**



## Ujumbe wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

*Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi,*
***Mbarak Abdulwakil***

Katika kipindi cha miaka 50 iliyopita, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imefanikiwa kwa kiwango kikubwa katika kulinda usalama wa raia na mali zao.

Hali hii inathibitishwa na kuwepo kwa amani na utulivu hapa nchini. Hali ya kuwepo na amani na utulivu nchini mwetu imetoa mchango mkubwa katika harakati za kuleta maendeleo katika nyanja mbalimmbali za kiuchumi na kijamii hususan tunapoadhimisha miaka 50 ya Uhuru wa Nchi yetu (Tanzania Bara).

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina majukumu mengi ikiwemo kulinda usalama wa raia na mali zao, kuhifadhi na kuwarekebisha wafungwa, kudhibiti utokaji na uingiaji nchini wa raia na wageni, kutoa huduma za zimamoto na uokoaji, kuwahudumia wakimbizi waliopo nchini, kutekeleza Programu ya Huduma kwa Jamii na kutoa Vitambulisho vya Taifa.

Mbali na mafanikio katika suala la ulinzi na usalama wa raia na mali zao pia tumefanikiwa kuboresha huduma katika magereza, ikiwemo huduma za afya, na malazi. Pia huduma nyingine zimeboreshwa ikiwa ni pamoja na huduma za uhamiaji, kwa mfano pasi ya kusafiria ambayo awali ingeweza kuchukua muda wiki tatu kupatikana, sasa inaweza kupatikana katika kipindi cha wiki moja au chini ya hapo kwa wale wenye shughuli za dharura.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inakabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo tatizo la kuongezeka kwa ajali za barabarani, uhamiaji haramu na biashara ya dawa za kulevya. Kwa kuwa amani na utulivu ni chachu ya kuleta maendeleo, ninatoa wito kwa wananchi wote waheshimu na kufuata sheria za nchi ili kudumisha amani na utulivu katika nchi yetu. Tumethubutu, tumeweza, tunazidi kusonga mbele.

Mbarak M. Abdulwakil
**KATIBU MKUU**

# MAFANIKIO YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 50 YA UHURU WA TANZANIA BARA (1961– 2011)

## HISTORIA YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

1. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iliundwa tarehe 15 Desemba mwaka 1961 baada ya Tanganyika kupata Uhuru. Kuanzishwa kwa Wizara hii kulilenga kuunda chombo ambacho kingesimamia masuala ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao katika mazingira ya nchi huru. Chombo hiki kimeiwezesha nchi yetu kuondokana na sera za kikoloni ambazo zilianzishwa kwa ajili ya kulinda maslahi ya wakoloni. Majukumu ya Wizara yalitekelezwa kwa kupitia Jeshi la Polisi na Idara ya Magereza.


### Jeshi la Polisi wakati wa Utawala wa Kijerumani 1886-1919

2. Utawala wa Kijerumani haukuanzisha Jeshi rasmi la Polisi badala yake Wajerumani walikuwa wakiwatumia watawala wa Vijiji (Maakida na Majumbe) katika kutekeleza majukumu ya kipolisi. Kwa upande mwingine Askari wa Jeshi na vikundi vingine vya ulinzi *(para–military groups)* vilitumika kudhibiti upinzani wa ndani pamoja na kulinda mipaka. Mnamo mwaka 1916 Wajerumani walianzisha Jeshi la Polisi la kiraia *(Civilian Police Force)* baada ya kuelekea kushindwa na majeshi ya Kiingereza katika Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, ili kulinda vitega uchumi, makazi ya Wajerumani na mipaka ya koloni la Tanganyika. Kikosi hiki cha Polisi kilichokuwa na askari 31 chini ya Meja S. T. Davies kutoka Afrika ya Kusini kilitekeleza majukumu ya kipolisi hadi mwaka 1919 Wajerumani waliposhindwa na Waingereza.

## Jeshi la Polisi wakati wa utawala wa Waingereza 1919-1961

3. Waingereza walianzisha taasisi mbalimbali ikiwemo Jeshi la Polisi lilojulikana kama *"Tanganyika Police Force and Prisons Service"* chini ya Sheria ya Jeshi la Polisi na Magereza ya mwaka 1919 *(The Police Force and Prisons Ordinance Cap.40)*. Tarehe 25 Agosti 1919 Serikali ya Kiingereza ilianzisha rasmi Jeshi la Polisi kupitia tangazo la gazeti la Serikali Na. 1.Vol. I Na. 21-2583. Makao Makuu ya Jeshi la Polisi yalikuwa Lushoto *(Wilemstal)* Tanga. Major S. T. Davies aliteuliwa kuwa Kamishna wa kwanza wa Jeshi hilo na baadaye nafasi yake ilichukuliwa na P. F. Brownie Esq aliyehamishwa kutoka Kenya. Tofauti na utawala wa Kijerumani, Jeshi hili lilipewa majukumu ya kipolisi, Magereza, Usalama wa Taifa, kimahakama na ya kiutawala pale ambapo hapakuwa na Maofisa Tawala au Wakuu wa Wilaya.

4. Ingawa Jeshi la Polisi lilijitenga na shughuli za kijeshi bado lilikuwa na jukumu la kulinda maslahi ya wakoloni wa Kiingereza. Hali hii ilijionesha kwenye muundo wa Jeshi la Polisi ambapo nafasi za juu zilishikwa na wazungu, nafasi za kati zilishikwa na Waasia na vyeo vya chini vilibaki kwa wazawa. Katika mwaka 1922 kulikuwa na Wazungu 68 wenye vyeo kuanzia Wakaguzi hadi Makamishna, Wakaguzi 25 wenye asili ya Asia na Waafrika 748 wa vyeo vya chini. Pamoja na kuongezeka kwa idadi ya Waafrika ndani ya Jeshi la Polisi, hali ya kubaguliwa iliendelea. Kwa mfano, mwaka 1930 Jeshi la Polisi lilikuwa na Wazungu 78 kwenye nafasi za juu, Waasia 67 kwenye vyeo vya kati na Waafrika 1719 kwenye nafasi za chini. Mbali na kushika nafasi za chini katika Jeshi la Polisi, Waafrika pia walibaguliwa kwa taratibu za kiutawala, makazi na stahili.



*Askari Polisi na mavazi yao wakati wa ukoloni*

5. Wakati wa Utawala wa Kiingereza shughuli za kipolisi zilifanywa kwenye maeneo ya miji na vijiji vilivyokuwa na idadi kubwa ya walowezi wa kizungu. Katika maeneo haya vituo vya polisi vya muda *(Detached Police Stations)* vilianzishwa kwa ajili ya kulinda mashamba ya walowezi. Katika kipindi cha Vita Kuu ya Pili ya Dunia (1939-1945) utawala wa Kiingereza ulipanua wigo wa ajira ndani ya Jeshi la polisi na kuongeza idadi ya Maofisa wa Kiafrika katika nafasi za kati na za juu. Mpaka kufikia mwaka 1960, kulikuwa na Waafrika 28 kwenye ngazi za juu za Jeshi la Polisi.

6. Kwa upande wa Zanzibar, Jeshi la Polisi lilianzishwa mwaka 1873 kwa ajili ya kusimamia sheria za kupinga biashara ya utumwa. Jeshi hili lilijumuisha askari wa Kiingereza na wa Sultani wa Zanzibar. Mwaka 1877 Serikali ya Kiingereza ilimteua Kamanda wa Kikosi cha Maji, Lloyd Mathews, kuongoza askari 1300 wakiwemo Waafrika 300. Mwaka 1907 wakati Zanzibar ikiwa chini ya uangalizi wa Waingereza *(Protectorate)*, Sultani alilivunja Jeshi la Polisi baada ya askari wake kugoma kutokana na mishahara midogo na mazingira duni ya kazi na kuunda Jeshi la Polisi lililojumuisha askari wa akiba kutoka Tanganyika.

**Jeshi la Polisi kuanzia mwaka 1961**

7. Baada ya Tanganyika kupata uhuru tarehe 9 Desemba 1961 jukumu la Jeshi la Polisi lilibadilika kutoka kusimamia maslahi ya kikoloni na kuwa jeshi la kusimamia utekelezaji wa sheria ndani ya Tanganyika huru. Kimsingi muundo na majukumu ya Jeshi la Polisi yalibaki kama yalivyo. Mabadiliko makubwa yaliyojitokeza wakati huo ni kuongezeka kwa Maofisa wa Kiafrika wenye vyeo vya juu ili kuchukua nafsi zilizokuwa zikishikiliwa na Wazungu. Hii ilikuwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya kuwapatia nafasi Waafrika katika Serikali *(Africanization Policy)*. Mwaka 1962 Elangwa Shaidi aliteuliwa kuwa Mwafrika wa kwanza kushika nafasi ya juu kabisa katika Jeshi la Polisi, ya Kamishna wa Polisi.

**Jeshi la Polisi mwaka 1964**

8. Baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964, majukumu na muundo wa Jeshi la Polisi yalibadilika hasa baada ya masuala ya ulinzi na usalama kuwa ya Muungano. Sheria za Jeshi la Polisi la Zanzibar zilifutwa na iliyokuwa Sheria ya Polisi ya Tanganyika ilianza kutumika Tanzania Bara na Zanzibar. Jeshi la Polisi lilianzisha nafasi ya Inspekta Jenerali wa Polisi na Elangwa N. Shaidi aliteuliwa kuwa Inspekta Jenerali wa Polisi wa kwanza. Katika kipindi hiki utendaji wa Jeshi la Polisi ulikwenda sambamba na mabadiliko ya sera za kisiasa. Kwa mfano, ilikuwa ni lazima kwa mtu anayetaka kuajiriwa ndani ya Jeshi la Polisi kuwa na kadi ya chama cha TANU au ASP. Jeshi la Polisi liliendelea kuwa sehemu ya chama tawala hadi Julai Mosi, 1992 baada ya kuanzishwa kwa Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa.

9. Jeshi la Polisi limeundwa kisheria na kupewa jukumu la kusimamia usalama wa raia na mali zao pamoja na kusimamia utekelezaji wa sheria za nchi. Majukumu ya Polisi yametajwa katika Kifungu cha 5 cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi

Cap.322 (R.E. 2002). Majukumu haya ni kuzuia na kupambana na uhalifu, kuwakamata wahalifu, kupeleleza makosa ya jinai, kuhakikisha sheria za nchi zinafuatwa na kudumisha amani ya nchi.


**Jeshi la Magereza wakati wa ukoloni**

10. Jeshi la Magereza lilianzishwa rasmi tarehe 25/8/1931 baada ya mgawanyiko wa Majeshi ya Polisi na Magereza. Kabla ya mwaka 1931 Jeshi la Polisi lilifanya pia kazi za Magereza kufuatana na madhumuni ya wakoloni. Wakati Jeshi la Magereza lilipoanzishwa liliitwa Idara ya Jela ambapo shughuli zake kubwa zilihusu kuwadhibiti wafungwa pamoja na kuwafanyisha kazi ngumu.
11. Sheria ya Magereza ya Mwaka 1933*(Prison Ordinance-Cap. 58)* iliwabagua wafungwa katika madaraja matatu kwa rangi zao. Daraja la Kwanza lilikuwa ni Wazungu, Daraja la Pili lilikuwa ni kwa ajili ya Wahindi, Waarabu, Machotara na Wasomali na Daraja la Tatu lilikuwa ni Waafrika. Sheria hiyo iliagiza kifungo kiambatane na kazi ngumu lakini kifungu hicho kilifutwa tarehe 18/2/1955 *(Imprisonment Reform Act - Cap.357)*. Kabla ya Jeshi la Polisi na Magereza halijatenganishwa mwaka 1931 maafisa 31 wa kwanza walikuwa Makaburu kutoka Afrika Kusini waliofika nchini mwaka 1916. Maafisa hawa wa Kikaburu walisifika sana kwa ukatili wao.

**Mafunzo ya Watumishi Wakati wa Ukoloni**

12. Kimsingi Mafunzo ya Askari yalizingatia kwata na ukakamavu wa mwili. Suala la uwezo wa kielimu halikupewa uzito unaostahili. Kwa hivyo, mafunzo hayakulenga urekebishaji wa wafungwa isipokuwa harubu na ukatili. Chuo cha kwanza cha Magereza wakati huo kilianzishwa Msasani, Dar es Salaam mwaka 1933. Chuo hiki kilihamishiwa Tabora mwaka 1949 na baadaye Ukonga, Dar es Salaam tarehe 1/8/1959. Askari

Jela wa Kiafrika walikuwa na hali ngumu wanapoingia chuoni. Askari Jela hawakuwa na viatu. Kwa hivyo, tangu chuoni askari alivaa sare zikiwa na patisi peke yake bila viatu hadi mwanzoni mwa mwaka 1959.



*Askari Jela wakiwakagua wafungwa kuhakikisha kuwa hawana vitu vinavyoweza kuhatarisha usalama gerezani*

**Jeshi la Magereza Baada ya Uhuru**

13. Mara baada ya Uhuru mwaka 1961, Serikali ilibadili sura na mwelekeo wa Magereza nchini kwa kuanzisha rasmi Sera ya Urekebishaji wa Wahalifu *(Rehabilitation of Prisoners)* ambayo iliwekwa wazi na Sheria Mpya ya Magereza ya Mwaka 1967 (*Prisons Act, 1967*). Sheria hii iliweka viwango vya kimataifa kuhusu Haki za Binadamu na Utunzaji wa Wafungwa. Falsafa ya urekebishaji ilianza kutekelezwa mwaka 1963 kwa uteuzi wa Kamishna wa Magereza, Mtanzania wa kwanza marehemu Obadia Rugimbana. Sheria Kuu ya Magereza Na. 34 ya mwaka 1967 na Kanuni zake za mwaka 1968 na 1969 zilianza kutumika katika uendeshaji wa Magereza chini ya uongozi wa Kamishna wa Magereza Bw. Ramadhani Nyamka ambaye aliongoza mwaka 1967 hadi 1977.

## Utawala na Uendeshaji wa Magereza

14. Kati ya mwaka 1964 na 1974 Mikoa iliongezwa kutoka majimbo 8 yaliyokuwepo kabla ya Uhuru hadi mikoa 20. Wakuu wa Magereza makubwa nane katika majimbo waliongezewa madaraka ya kuongoza Magereza katika zaidi ya mkoa mmoja. Wakuu hao walijulikana kama Mrakibu Msaidizi wa Mkoa, Mrakibu au Mrakibu Mwandamizi kufuatana na cheo cha Afisa husika. Mgawanyo wa mikoa hiyo ulikuwa:-

| | | |
|---|---|---|
| Mashariki | - | Pwani na Morogoro |
| Magharibi | - | Tabora na Kigoma |
| Ziwa | - | Mwanza, Kagera, Mara na Shinyanga |
| Kati | - | Dodoma na Singida |
| Kaskazini | - | Kilimanjaro na Arusha |
| Kusini | - | Mtwara, Ruvuma na Lindi |
| Nyanda za Juu | - | Iringa na Mbeya |
| Tanga | - | Tanga |

15. Mwaka 1974 Jeshi lilianza kuongozwa na Kamishna Mkuu wa Magereza badala ya Kamishna wa Magereza. Kamishna Mkuu wa Kwanza alikuwa Ramadhani Nyamka. Wakuu wa Magereza wa Mikoa waliteuliwa kusimamia uendeshaji wa Magereza katika kila mkoa. Maafisa hao walipewa Cheo cha Kamishna Msaidizi wa Magereza. Ofisi ya Makao Makuu ya Magereza ilipanuliwa ili kujumuisha sehemu kuu nne ambazo ni Utawala, Ujenzi, Kilimo na Mifugo na Viwanda. Baadaye sehemu kuu mbili zaidi ziliongezwa. Sehemu hizo ni Sheria na Urekebishaji na Ustawi wa wafungwa.

16. Kabla ya mwaka 1983, idadi ya Maafisa na Askari wa Magereza ilikuwa watumishi 5,000 ambao hawakukidhi mahitaji. Hivi sasa Jeshi lina Watumishi 13,000. Mwaka 1990 Wizara ya Mambo ya Ndani ilianzisha Tume ya Polisi na Magereza chini ya Sheria ya Jeshi la Polisi na Tume ya Huduma za Magereza Na. 8 ya mwaka 1990 (*The Police*

*Force and Prisons Service Commission Act, No.8 of 1990)* kwa ajili ya kushughulikia malalamiko ya askari. Jeshi pia lilitunga Kanuni za Utumishi wa Magereza mwaka 1997 *(Prisons Service Regulations, 1997)* ili kuimarisha maslahi ya kazi ambayo awali yalisimamiwa na Sheria ya Utumishi wa Umma, 1962 (Civil Service Act, 1962) na Kanuni za Huduma za Magereza (Prisons Service - Civil Service – Regulations) za mwaka 1969.

## Muundo na Majukumu ya Jeshi la Magereza

17. Mwaka 1992 Jeshi liliundiwa Divisheni tatu chini ya Kamishna Mkuu wa Magereza. Kila divisheni ikiongozwa na Kamishna. Divisheni hizo ni Fedha na Utawala, Uzalishaji Mali na Sheria na Uendeshaji wa Magereza. Kutokana na Uboreshaji wa Utumishi wa Umma kati ya mwaka 1993 hadi 1997, Muundo wa Jeshi la Magereza ulifanyiwa marekebisho. Divisheni ya Uzalishaji Mali ilibadilishwa na kuwa Divisheni ya Huduma za Urekebishaji.

## Uongozi katika Ngazi ya Mikoa

18. Katika mikoa kuna Wakuu wa Magereza wa Mikoa na chini yao Wakuu wa Magereza Makubwa ya Ngome *(Central Prisons)*, Magereza ya Wazi ya Kilimo *(Open Farm Prisons)*, Magereza ya Wilaya *(District Prisons)* na Kambi za Magereza *(Prison Camps)*. Magereza ya Ngome yapo 12 na huweka wafungwa wa aina zote. Magereza Makubwa ya Wazi yapo 46 na yanahifadhi wafungwa wanaotumikia kifungo kisichozidi miaka 10. Magereza ya Wilaya yapo 68. Magereza haya yanahifadhi mahabusu na wafungwa wa miaka isiyozidi 10. Makambi ya Magereza huanzishwa kwa kazi maalum na huweka wafungwa wa miezi isiyozidi 12. Kwa sasa Tanzania ina makambi 40.

19. Hivi sasa kuna gereza moja tu la Wanawake. Gereza hilo ni gereza la Kingolwira (Morogoro). Wafungwa wa kike

pia wanahifadhiwa kwenye sehemu za wanawake kwenye Magereza ya Ngome na Magereza ya Wilaya nchini kote. Aidha, kuna Gereza Maalum la Vijana Wami, Morogoro kwa ajili ya wafungwa wa umri chini ya miaka 21 na Gereza la Wahalifu wenye matatizo ya akili Isanga (Dodoma) *(Therapeutic Institution for Criminal Lunatics)*.

20. Jeshi la Magereza lina vyuo vinne. Vyuo hivi ni Chuo cha Maafisa wa Magereza Ukonga, Chuo cha Mafunzo ya Awali Kiwira, Chuo cha Ufundi Stadi Ruanda, na Chuo cha Ufundi Magari na Udereva Kingolwira.



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mbarak Abdulwakil akikagua Gwaride la Kufunga Mafunzo ya Uongozi katika Chuo cha Magereza Kiwira, Mbeya*

## Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

21. Huduma ya Zimamoto na Uokoaji Tanzania Bara ilianza baada ya vita vya pili vya Dunia. Kwa upande wa Zanzibar shughuli hizi zilianza mwaka 1930. Hapo awali kikosi hicho kiliitwa Brigedi ya Polisi ya Zimamoto *"Police Fire Brigade"*. Wakati wa utawala wa Kiingereza kikosi hiki kilianzishwa kutokana na uelewa wao

wa madhara ya moto yaliyokuwa yamewakumba huko kwao. Kituo cha kwanza cha Zimamoto kilikuwa katika eneo zilipo Ofisi za Polisi Usalama Barabarani, Dar es Salaam. Kikosi hiki kilipoanzishwa kilifanya kazi katika mazingira magumu. Kikosi hakikuwa na vifaa vya kukabiliana na majanga ya moto na vya mafunzo. Kwa kuwa kuchanganywa kwa kazi za Polisi na Zimamoto kuliathiri shughuli za Zimamoto, Serikali ya Kikoloni iliamua kutenganisha shughuli hizo mwaka 1950. Huduma za kuzimamoto iligawanywa katika makundi yafuatayo:-

(i) Zimamoto ya Manispaa chini ya usimamizi wa Manispaa.
(ii) Zimamoto ya Kiwanja cha Ndege chini ya usimamizi wa Idara ya Kazi.

22. Baada ya Muungano Serikali iliamua Zimamoto zote nchini ziwe chini ya mwajiri mmoja yaani Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Waraka wa Baraza la Mawaziri Namba 37. Mwaka 1985 Bunge lilipitisha Sheria Na. 3 ya mwaka 1985 ya kuanzisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili huduma ya Zimamoto na Uokoaji zitolewe katika misingi ya nidhamu za Kijeshi. Ili kuboresha shughuli za Zimamoto na Uokoaji Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2007 lilipitisha sheria ya Zimamoto na Uokoaji *(The Fire and Rescue Force Act, No. 14 ya 2007)*. Kupitishwa kwa Sheria hii kulisababisha kutungwa kwa Kanuni za Utumishi *(Service Regulation)* na Kanuni za Ukaguzi za Usalama wa Moto *(Fire Safety Inspection Regulations)*, za mwaka 2008.

## Idara yaUhamiaji

23. Masuala ya udhibiti wa wahamiaji yalianzishwa mwaka 1924 chini ya Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 1924 *"Immigration Ordinance Cap 37 of 1924"* ili kusimamia uhamiaji ndani ya Tanganyika. Sheria hiyo ilianza kutumika tarehe 1, Februari 1925. Kuanzia mwaka 1924 hadi mwaka 1948, shughuli za udhibiti wa wahamiaji na utoaji wa pasipoti zilifanywa na kitengo maalum ndani ya Idara ya Polisi. Idara ya Uhamiaji

ilianzishwa rasmi tarehe 13 Julai, 1949. Hata hivyo, kutokana na uchache wa watumishi, Idara hiyo iliendelea kuwa chini ya Kamishna wa Polisi hadi alipoteuliwa rasmi Afisa Uhamiaji Mkuu (*Principal Immigration Officer)* kuongoza Idara hiyo. Mwezi Oktoba, 1949 Idara ilibadilishwa jina na kuitwa Idara ya Uhamiaji na Pasipoti *(Immigration and Passport Department)*.

24. Kuanzishwa kwa Idara ya Uhamiaji kulikuwa na lengo la kuimarisha udhibiti wa wageni waliokuwa wakiingia ndani ya Koloni la Tanganyika chini ya utawala wa Kiingereza hususan wazungu waliokuwa na makoloni mengine ndani ya Afrika pamoja na raia wa mataifa rafiki. Waafrika waliruhusiwa kutoka sehemu moja hadi nyingine bila udhibiti kutokana na mahitaji ya wafanyakazi "manamba" kwenye mashamba ya wakoloni. Aidha, baada ya kuanza vuguvugu la kudai uhuru katika baadhi ya mataifa ya Afrika katika miaka ya 1950, baadhi ya makabila kama Wakikuyu, Wakamba na Wajaluo kutoka Kenya walidhibitiwa kuingia ndani ya koloni la Tanganyika ili kuzuia kuenea kwa harakati za kudai Uhuru kwa nguvu kama zilivyokuwa huko Kenya.

**Majukumu ya Idara ya Uhamiaji baada ya Uhuru**

25. Baada ya Tanganyika kupata uhuru kutoka kwa wakoloni wa Kiingereza tarehe 09 Desemba, 1961, Idara iliendelea kuitwa Idara ya Uhamiaji na Pasipoti. Majukumu ya Idara yaliongezeka. Hata hivyo majukumu hayo yalikuwa ni utoaji wa Viza kwa wageni walioomba kuingia Tanganyika kwa shughuli mbalimbali, kufanya misako, doria pamoja na shughuli nyingine za upelelezi. Katika kutekeleza majukumu hayo, Idara iliongozwa na Sheria ya Uraia Na. 3 ya Mwaka 1961 *(The Tanganyika Citizenship Act.of 1961, CAP 512)* na Sheria ya Uraia ya Na. 15 ya Mwaka 1962 *(The Tanganyika Citizenship Act No.15 of 1962)*. Sheria hizi zilifutwa na Sheria ya Uraia No. 6 ya mwaka 1995 (The Tanzania Citizenship Act No 6 1995). Aidha, masuala ya uhamiaji yalisimamiwa na Sheria ya

Uhamiaji ya mwaka 1961 *(Immigration Ordinance of 1961)* iliyofutwa na sheria Na. 41 ya mwaka 1963 (Immigration Act No. 41 of 1963). Vile vile Sheria ya Uhamiaji Na. 8 ya mwaka 1972 *(The Immigration Act No 8 Of 1972)* pia ilifutwa na Sheria ya Uhamiaji ya Na.7 ya 1995.

**Majukumu ya Idara ya Uhamiaji baada ya Muungano**

26. Baada ya Muungano, majukumu ya Idara ya Uhamiaji yaliendelea kuwa yale yale, isipokuwa shughuli hizo zilipanuka kufuatia Muungano wa Tanganyika na Zanzibar . Kwa upande wa Tanzania Bara, utendaji kazi wa Idara ya Uhamiaji kuhusu masuala ya uraia uliendelea kusimamiwa na Sheria ya Uraia Na. 3 ya Mwaka 1961 *(The Tanganyika Citizenship Act. No. 3 of 1961)* na Sheria ya Uraia ya Mwaka 1962 *(The Tanganyika Citizenship act No 15 of 1962.* Kwa upande wa Zanzibar, masuala ya Uraia yalisimamiwa na Sheria ya Uraia ya Zanzibar (The Zanzibar Nationality Decree of 1952) ambazo zilifutwa na sheria ya uraia ya mwaka 1995 (the Tanzania Citizenship Act No 6. of 1995). Masuala ya udhibiti wa wahamiaji yaliendelea kusimamiwa na Sheria ya Uhamiaji *(Immigration Ordinance of 1961)* iliyofutwa na sheria Na. 41 ya mwaka 1963 *(Immigration Act No. 41 of 1963)* ambayo pia ilifutwa na Sheria ya Uhamiaji Na. 8 ya Mwaka 1972 *(The Immigration Act No. of 1972)*. Majukumu ya Idara ya Uhamiaji yalisimamiwa na Tamko la Kanuni na Udhibiti wa Uhamiaji la mwaka 1923 *(Immigration Regulation and Restriction Decree, Cap 43 of 1923)* huko Zanzibar.

27. Mwaka 1995 sheria zilizokuwa zinasimamia majukumu ya uhamiaji, Tanzania bara na Zanzibar zilifutwa na kutungwa Sheria mpya ya Uhamiaji Na. 7 ya Mwaka 1995 na Kanuni zake za mwaka 1997. Aidha, sheria zilizokuwa zinasimamia masuala ya Uraia ziliunganishwa na kuwa Sheria ya Uraia Na. 6 ya Mwaka 1995 na Kanuni zake za Mwaka 1997. Ili kuboresha huduma za pasipoti, Serikali ilitunga Sheria ya kusimamia utoaji wa Pasipoti na Hati za Safari mwaka 2002 *(Tanzania Passport and Travel Document Act No. 20 of 2002)* na Kanuni zake za mwaka 2004.

**Idara ya Wakimbizi**

28. Idara ya Wakimbizi ilianzishwa rasmi mwaka 1997. Idara hii ilitungiwa Sheria ya Wakimbizi Na. 9 ya mwaka 1998 kwa madhumuni ya kusimamia na kuratibu masuala yote yanayohusu wakimbizi. Kabla ya kuundwa kwa Idara hii shughuli zake zilikuwa zikifanywa na Kitengo chini ya Ofisi ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

29. Wakimbizi walianza kuingia nchini kuanzia miaka ya 1940 kwa vikundi vidogo vidogo na kuishi na wenyeji. Hata hivyo, wimbi kubwa la kwanza la wakimbizi kuingia Tanganyika lilikuja mwaka 1959 kutoka Rwanda. Kundi hili lilikuwa la kabila la Watutsi ambao walikuwa wakikimbia machafuko yaliyotokea Rwanda baada ya migogoro ya chama cha Kitutsi (*Union Nationale Rwandaise*) na chama cha Kihutu (*Parmehutu*). Kutokana na mgogoro huo, Umoja wa Mataifa mwaka 1961 ulisimamia uchaguzi, ambao uliwezesha chama cha Kihutu (*Parmehutu Party*) kushinda uchaguzi.

30. Baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 26 Aprili 1964, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhia Mkataba wa Kimataifa kuhusu Hadhi ya Wakimbizi (*The 1951 Geneva Convention on the Status of Refugees*). Uamuzi huu ulipelekea kufunguliwa kwa Ofisi ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) hapa nchini tarehe 12 Mei 1964. Kuanzia mwaka 1961 hadi 1965 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haikuwa na Sheria yoyote ya kuhudumia Wakimbizi bali kulikuwa na miongozo na matamko mbalimbali ambayo yalikuwa yanatolewa na viongozi wa juu wa Serikali ambayo yalisisitiza umoja wa Afrika.

31. Tanzania ilikuwa ni kitovu na makao makuu ya harakati za ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika. Nchi ya Tanzania ilijiona ina wajibu wa kuwapokea wakimbizi kwa sababu iliamini kuwa uhuru wa Tanzania haukuwa na maana mpaka

Afrika yote iwe huru. Ndio maana Tanzania iliwahifadhi wapigania uhuru kutoka nchi mbalimbali zikiwemo Msumbiji, Afrika Kusini, Zimbabwe, Angola, na Namibia. Kutokana na hali hiyo, Tanzania imehifadhi wakimbizi wengi kutoka nchi hizo na sehemu zingine kwa nyakati tofauti. Baada ya kupatikana uhuru wa nchi hizo wakimbizi hao walirejea katika nchi zao za asili. Tanzania iliendelea kupokea wakimbizi kwa nyakati tofauti. Kutokana na migogoro ya kisiasa.

**Hifadhi ya wakimbizi kwenye Makazi 1960 – 1980**

32. Katika kipindi hiki, makundi ya wakimbizi yaliendelea kuingia nchini. Mfano kundi la pili la wakimbizi baada ya lile la mwaka 1959, lilikuja Tanzania mwaka 1964. Wakimbizi wapatao elfu tatu (3000) waliingia Tanzania kutoka Rwanda. Wakimbizi hawa walitoka jimbo la Kivu nchini Zaire ambako walikimbilia awali na baadaye kuletwa Tanzania kwa makubaliano na UNHCR. Hivyo kufikia mwishoni mwa mwaka 1965 kulikuwa na wakimbizi wapatao 15,000 kutoka Rwanda. Wakimbizi wa Rwanda waliokuwa wanaishi katika mikoa ya Kagera na Rukwa, walipewa uraia mwaka 1980 na kupelekea makazi yao kufungwa.

33. Mwaka 1964 lilitokea wimbi lingine la wakimbizi kutoka Msumbiji baada ya Chama cha FRELIMO kuanzisha harakati dhidi ya ukoloni wa Kireno ambapo wakimbizi wapatao 10,000 walikimbilia Tanzania toka nchini humo. Wakimbizi hao walirejea kwao mwaka 1975 baada ya Msumbiji kupata uhuru. Wakimbizi wa Msumbiji walianza tena kukimbilia nchini mwaka 1986 baada ya kuzuka vita nchini humo kati ya majeshi ya Serikali na ya RENAMO. Wakimbizi hao walirejea nchini Msumbiji katika miaka ya 1990.

34. Mwaka 1972 wakimbizi wengine waliingia Tanzania kutokea Burundi kufuatia vurugu za uasi nchini humo. Kundi hili lilikuwa na wakimbizi wapatao 130,000, wengi wao wakiwa wa jamii

ya Kihutu. Hali hii ilisababisha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzisha Makazi ili wakimbizi waweze kuwa na sehemu ya kuishi na kuendesha shughuli zao hasa za kilimo. Sera ya wakati huo iliruhusu wakimbizi kupewa ardhi kwa ajili ya makazi na shughuli za kilimo. Aidha, Jumuiya ya Kimataifa kupitia UNHCR ilijenga miundo mbinu mbalimbali kwenye maeneo hayo kama vile Shule, Zahanati na Barabara ili wakimbizi waweze kuishi maisha mazuri. Kutokana na kuwepo wakimbizi hawa wa Burundi, mnamo mwaka 1972 Makazi ya Wakimbizi ya Ulyankulu, katika Wilaya ya Urambo, mkoani Tabora, yalianzishwa kwa ajili ya wakimbizi hawa. Mwezi Agosti, mwaka 1973 yalianzishwa Makazi ya Katumba, katika wilaya ya Kasulu, mkoani Kigoma, na makazi ya Mishamo, ambayo pia yalikuwa wilayani Kasulu, yalianzishwa mwanzoni mwa mwaka 1978.

35. Jumuiya za Kimataifa kupitia UNHCR na mashirika ya kimataifa yanayohusu misaada ya kibinaadamu, walitoa huduma kwa wakimbizi hawa hadi tarehe 28 Juni 1980 yalipokabidhiwa rasmi kwa Serikali baada ya kuonekana kuwa wakimbizi walikuwa wakijitosheleza kwa chakula na huduma nyingine za kijamii. Awali, Makazi ya Katumba yalikabidhiwa kwa Serikali mwezi Juni 1978 yakiwa na wakimbizi 60,000. Makazi ya Mishamo yalipoanzishwa yalikuwa na wakimbizi wapatao 37,000.

36. Mwaka 1993 kulitokea jaribio la kupindua Serikali nchini Burundi ambalo lilisababisha wakimbizi wapatao 300,000 kukimbilia Tanzania baada ya kuuawa kwa Rais wa Kwanza wa Burundi aliyechaguliwa kidemokrasia, Melchior Ndadaye ambaye aliuawa tarehe 21 Oktoba 1993. Vilevile katika nchi ya Rwanda, miaka 1990 kulizuka mapigano ya waasi wa *Rwandese Patriotic Front (RPF)* na Serikali ya Rais Habyarimana ambaye alifariki kwa ajali ya ndege pamoja na Rais wa Burundi Aprili 1994 na kusababisha wakimbizi wa Rwanda wapatao zaidi ya milioni moja kuingia nchini kuomba hifadhi

ya ukimbizi. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 1995 kulikuwa na wakimbizi wapatao 700,000 kutoka Rwanda.

37. Kwa kuwa idadi ya Wakimbizi iliongezeka sana Serikali ya Tanzania iliamua kubadili sera ya kupokea na kuhifadhi wakimbizi. Badala ya kuwaweka kwenye Makazi na kuwagawia hekta mbili na nusu za ardhi kwa kila familia, walipangiwa kuishi kwenye maeneo maalum ya makambi yaliyotengwa kisheria *(designated areas)* na kupatiwa huduma zote za kibinadamu ikiwemo chakula, dawa, malazi na huduma hizi zilitolewa na Jumuiya ya Kimataifa kupitia UNHCR. Tofauti ya Makazi na Makambi ni kuwa katika makazi wakimbizi hupewa ardhi kwa ajili ya kujikimu na kujihudumia wenyewe bila msaada wa Serikali au mashirika ya kimataifa, na huendesha shughuli zao za kujipatia chakula na huduma zingine za jamii, wakati makambi ni maeneo maalum kwa ajili ya wakimbizi ambao hupewa eneo la mita 1600 za mraba kwa ajili ya kujenga makazi yao na kwa ajili ya bustani ndogo ndogo *(kitchen gardening)* na hupatiwa huduma nyingine zote na UNHCR kwa kushirikiana na mashirika yanayotoa misaada ya kibinadamu. Kambi ya Benaco iliyokuwepo wilayani Ngara na kuhifadhi wakimbizi 250,000 ndiyo iliyokuwa kambi kubwa zaidi duniani kwa kuhifadhi idadi kubwa ya wakimbizi kwa wakati huo. Wakimbizi wa Rwanda walirejea kwao kwa hiari mwishoni mwa mwaka 1997.

38. Kubadilishwa kwa sera ya maeneo ya kuishi wakimbizi ilipelekea kubadilishwa kwa Sheria ya Wakimbizi Na. 2 "*The Refugees Control Act No.2*" ya mwaka 1966. Serikali ya Tanzania kupitia Bunge lake ilitunga Sheria mpya Na. 9 ya Wakimbizi ya mwaka 1998. Hadi kufikia Desemba, 2010 idadi ya wakimbizi nchini ilikuwa 109,286. Wakimbizi hawa walitoka Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Somalia na mataifa mengine ya Rwanda, Uganda, Sudan, Ethiopia na Zimbabwe. Mchanganuo wa idadi hii ni kama ifuatavyo: Burundi 47,350, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo 60,186,

Somalia 1,488, Mataifa mengine 262. Aidha, mwaka 2010 jumla ya wakimbizi 162,256 walipewa uraia wa Tanzania.

39. Makambi yaliyokuwepo nchini ambayo baadhi yamefungwa na mengine bado yapo hadi sasa ni kama ifuatavyo:-

| Na. | Kambi | Mwaka wa kuanzishwa | Wilaya ilipo/ ilipokuwa | Nchi walikotoka | Idadi ya Wakimbizi | Hali ya sasa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 01 | Mkugwa | 1994 | Kibondo | Rwanda, Burundi, Uganda, Somalia, Ethiopia, Kenya, DRC, Sudan, Madagascar | 3,000 | Imefungwa tarehe 26/11/2007 |
| 02 | Lukole A & B | 1993 | Ngara | Burundi | | Imefungwa 1997 |
| 03 | Kitali | 1994 | Biharamulo | Burundi | 8,004 | Imefungwa 2001 |
| 04 | Lugufu I & II | 1997 | Kigoma vijijini | DRC | 85,373 | Lugufu I imefungwa 2009 na Lugufu II imefungwa 31/09/2007 |
| 05 | Nyarugusu | 1996 | Kasulu | DRC | 38,438 | Inaendelea |
| 06 | Muyovosi | 1993 | Kasulu | Burundi | 35,710 | Imefungwa 2006 |
| 07 | Kanembwa | 1993 | Kibondo | Burundi | 1212 | Imefungwa 18/05/2007 |
| 08 | Mtendeli | 1993 | Kibondo | Burundi | - | Imefungwa 2006 |
| 09 | Karago | 1997 | Kibondo | Burundi | 4,227 | Imefungwa 2005 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 10 | Nduta | 1993 | Kibondo | Burundi | 35,534 | Imefungwa 2008 |
| 11 | Mtabila I & II | 1994 | Kasulu | Burundi | 36,459 | Inaendelea |
| 12 | Mkuyu | 1989 | Handeni | Somalia | | Imefungwa 2003 |
| 13 | Benaco | 1994 | Ngara | Rwanda | 250,000 | Imefungwa 1996 |
| 14 | Msuhura | 1994 | Ngara | Rwanda | 120,000 | Imefungwa 1996 |
| 15 | Lumasi | 1994 | Ngara | Rwanda | 100,000 | Imefungwa 1996 |
| 16 | Kagenyi | 1994 | Ngara | Rwanda | 30,000 | Imefungwa 1996 |
| 17 | Rubwera | 1994 | Karagwe | Rwanda | 60,000 | Imefungwa 1996 |
| 18 | Murongo | 1994 | Karagwe | Rwanda | 10,000 | Imefungwa 1995 |
| 19 | Chabalisa | 1994 | Karagwe | Rwanda | 120,000 | Imefungwa 1996 |
| 20 | Umukaliro | 1995 | Karagwe | Rwanda | 10,000 | Imefungwa 1996 |

## Idara ya Huduma kwa Jamii

40. Idara ya Huduma kwa Jamii *(Probation and Community Service Department)* imeanzishwa kufuatia muundo mpya wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tarehe 4 Julai, 2008. Mabadiliko hayo yaliipandisha hadhi iliyokuwa Sekretarieti ya Huduma kwa Jamii *(Community Service Secretariet)*. Kuanzishwa kwa Sheria ya Huduma kwa Jamii ni matokeo ya mapendekezo ya Tume ya Kurekebisha Sheria kuhusu kutafuta njia ya kupunguza msongamano wa wafungwa Magerezani. Mapendekezo haya yaliitaka Wizara ianzishe Programu ya Huduma kwa Jamii kama adhabu mbadala wa kifungo gerezani. Kwa kuzingatia mapendekezo haya Serikali ilipeleka muswada wa Sheria Bungeni na Bunge likapitisha Sheria ya Huduma kwa

Jamii Na. 6 ya mwaka 2002. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilichagua mikoa ya majaribio. Mikoa iliyochaguliwa kwa majaribio ilikuwa ni Dar es salaam, Dodoma, Mtwara, Kilimanjaro, Mwanza na Mbeya. Baada ya kupata uzoefu kutoka katika mikoa ya majaribio Sheria ya Huduma kwa Jamii ilianza kutekelezwa katika mikoa mingine ya Tanzania Bara. Mikoa hiyo ni Iringa, Tanga, Arusha, Kagera, Shinyanga na Mara.

**Idara ya Kushughulikia Malalamiko**

41. Idara ya kushughulikia Malalamiko ambayo awali ilijulikana kama Idara ya Ufuatiliaji Usalama wa Raia iliundwa tarehe 18 Aprili, 2007 baada ya kuanzishwa kwa iliyokuwa Wizara ya Usalama wa Raia. Wizara hii ilikuwa na Idara Kuu mbili ambazo ni Jeshi la Polisi na Idara ya Ufuatiliaji Usalama wa Raia. Kulingana na muundo wa wakati huo, Idara ilikuwa na Vitengo vitatu ambavyo ni Kitengo cha Malalamiko ya Wananchi, Polisi Jamii na Uhusiano wa Kimataifa. Baada ya Wizara ya Usalama wa Raia kuunganishwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi mwezi Februari 2008, Idara ilibadilishwa jina na kuitwa Idara ya Kushughulikia Malalamiko. Kwa sasa Idara ina Vitengo viwili ambavyo ni Kitengo cha Malalamiko na Kitengo cha Sheria na Utafiti.

**Idara ya Huduma za Sheria**

42. Idara ya Huduma za Sheria katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ilianzishwa rasmi tarehe 4 Julai, 2008 baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusaini Muundo mpya wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kabla ya hapo, ilifahamika kama Kitengo cha Sheria na Usajili wa Vyama vya Kijamii. Kazi kubwa ya Idara ni kutoa huduma za kisheria na pia kusajili Vyama vya Kijamii.

43. Usajili wa Vyama vya Kijamii unafanywa chini ya Sheria ya Vyama, Sura 337 ya mwaka 1954 kama ilivyorekebishwa kwa nyakati mbalimbali na kujadiliwa mwaka 2002 *(Societies Act Cap. 337 R.E 2002)*. Sheria hii ilitungwa kwa lengo la

kuandikisha na kusimamia vyama vyote vya kijamii kwa wakati huo, ikiwa ni pamoja na vyama vya siasa. Usajili na Usimamizi wa Vyama hivi pamoja na uwajibikaji wake unafanywa na Msajili wa Vyama chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa mujibu wa Sheria inayohusika, taratibu, masharti na kanuni za uendeshaji wa Vyama hivi pamoja na wajibu na majukumu ya Msajili kwa upande mmoja, na wa Vyama vyenyewe kwa upande mwingine, vimebainishwa ndani ya Sheria hiyo.

Baada ya Tanganyika kupata Uhuru mwaka 1961, mfumo wa siasa nao ulibadilika na nchi ikawa na mfumo wa siasa wa Chama kimoja. Sheria mbalimbali, ikiwemo ya Vyama, zilifanyiwa marekebisho. Baadhi ya marekebisho yaliyofanywa kwenye Sheria ya Usajili ni pamoja na kuondoa baadhi ya vyama kutoka kwenye usimamizi wa sheria hiyo na kuvihamisha kwenda Mamlaka na Taasisi nyingine zilizopewa jukumu hilo na kutekeleza na kusimamia sheria hizo. Sambamba na mabadiliko haya Wasajili mbalimbali waliteuliwa ikiwa ni pamoja na :-

1. Msajili wa Vyama vya Michezo chini ya Sheria ya Michezo,
2. Msajili wa Vyama vya Muziki na Burudani,
3. Msajili wa Vyama vya Siasa ambaye aliteuliwa baada ya kurudishwa kwa mfumo wa vyama vingi hapa nchini mwaka 1992 chini ya Sheria ya Vyama vya Siasa.

Kutokana na maendeleo hayo, vyama vilivyobaki chini ya usimamizi wa Sheria ya Vyama ni vya makundi yafuatayo:-

1. Vyama vya Dini,
2. Vyama vya Maendeleo ya Kijamii (Community Based).
3. Vyama vya Starehe na Burudani (Social Clubs).
4. Vyama vya Kimataifa (International Societies).
5. Vyama vyenye mwelekeo wa Kitaalamu (Professional Associations).

**Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa**

44. Wazo la kuunda Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa lilitokana na kikao cha Usalama '*Interstate Intelligence Gathering*' kilichofanyika mwaka 1968 kilichojumuisha wajumbe kutoka

nchi za Tanzania, Kenya, Uganda na Zambia. Kwa wakati huo nchi za Kenya na Zambia tayari zilikuwa na Vitambulisho vyao vya Taifa. Katika kikao hicho wajumbe waliazimia kwamba lazima nchi za Uganda na Tanzania nazo zitoe Vitambulisho vya Taifa kwa Raia wao ili kuimarisha uhusiano na usalama. Baada ya kikao hicho kumekuwa na jitihada mbalimbali za Serikali kuhakikisha Watanzania na wageni wote wanapatiwa Vitambulisho vya Taifa, lakini jitihada hizo hazikuweza kuzaa matunda yaliyotarajiwa kwa kipindi kirefu.

Mwaka 1986 Serikali ilitunga Sheria ya Vitambulisho ambayo haikutumika. Aidha Baraza la Mawaziri katika Kikao cha tarehe 3 Februari,. 2007 lilitoa mwongozo kuwa iundwe Kamati ya Usimamizi *(Steering Committee)* ya Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara na Vitengo vinavyohusika na mambo muhimu kuhusu Vitambulisho vya Taifa. Kamati hii pamoja na mambo mengine itakuwa na jukumu la kutoa mwongozo na mwelekeo wa program za Mradi. Hatimaye, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, alitia saini Hati ya kuidhinisha kuanzishwa kwa chombo cha kusimamia Vitambulisho vya Taifa kinachojulikana kama Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*National Identification Authority*). Hati hii imechapishwa katika Gazeti la Serikali, GN No.122 ya tarehe 01/08/2008.

45. Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa itatoa vitambulisho vya Taifa kwa Watanzania waliofikia umri wa miaka 18 na wageni wanaoishi nchini. Jumla ya watu kati ya milioni 25 na 26 wanatarajiwa kupatiwa vitambulisho hivyo. Hivi sasa Mamlaka ya Vitambulisho imeshakamilisha taratibu za kupata viwanja vya kujenga ofisi katika Wilaya zote za Tanzania Bara isipokuwa Wilaya za Ilala na Kinondoni. Mradi huu utagharimu shilingi bilioni 355 mpaka kumalizika kwake katika kipindi cha miaka mitano. Mradi wa Vitambulisho vya Taifa utakapomalizika utasaidia kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali kutoka walipa kodi 1,570,000 hadi 12,000,000, kukabiliana na tatizo la watumishi hewa Serikalini, kuwatambua wanafunzi wanaostahiki kupewa mikopo ya elimu ya juu na vyombo vya fedha, kuimarisha usalama na kuwatambua wapiga kura halali katika daftari la kudumu la wapiga kura.

## MUUNDO WA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

### Kuanzishwa kwa Wizara ya Usalama wa Raia

46. Baada ya Serikali ya awamu ya nne kuingia madarakani Jeshi la Polisi liliondolewa kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kuundiwa Wizara mpya ya Usalama wa Raia ambayo ilipewa jukumu pekee la kutekeleza shughuli za usalama wa raia na mali zao. Hata hivyo, tarehe 12 mwezi Februari mwaka 2008, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete alifanya tena mabadiliko ya Wizara ambapo Wizara ya Usalama wa Raia iliunganishwa tena na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kuitwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

47. Hivi sasa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina Idara za kiutendaji saba ambazo zinahusika moja kwa moja na utekelezaji wa majukumu ya wizara, ambazo ni:

1. Jeshi la Polisi
2. Jeshi la Magereza
3. Idara ya Uhamiaji
4. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji
5. Idara ya Wakimbizi
6. Idara ya Huduma kwa Jamii
7. Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa

Idara za Huduma ni:

- Idara ya Utawala na Rasilimali Watu,
- Idara ya Sera na Mipango,
- Idara ya Kushughulikia Malalamiko,
- Idara ya Huduma za Sheria.

Vitengo vya Wizara ni:

- Fedha na Uhasibu,
- Ukaguzi wa Ndani wa Hesabu,
- Teknolojia ya Habari na Mawasiliano,
- Ugavi na Manunuzi,
- Mawasiliano ya Serikali.

## Viongozi wa sasa wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi



*Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi,*
**Mhe. Shamsi Vuai Nahodha**



*Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi,*
**Mhe. Balozi Khamis Kagasheki**




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi,*
**Mbarak Abdulwakil**



*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi,*
**Mwamini Malemi**

## *MUUNDO WA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI*



## MAJUKUMU YA WIZARA

48. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina jukumu la kulinda usalama wa raia na mali zao. Katika kufanikisha utekelezaji wa jukumu hilo Wizara hii ina wajibu ufuatao:

(i) Kusimamia Usalama wa Raia na mali zao, Uchunguzi wa Makosa ya Jinai na Operesheni mbalimbali.

(ii) Kusimamia masuala ya Huduma za Magereza, Huduma za Uhamiaji, Huduma za Wakimbizi, Huduma za Zimamoto na Uokoaji, Huduma za Usimamizi na Uratibu wa Vyama visivyo vya Kiserikali.

(iii) Kuboresha utendaji kazi na maendeleo ya Rasilimali watu.

(iv) Kusimamia Idara zinazojitegemea, Mashirika na Miradi iliyo chini ya Wizara.

(iv) Kusimamia Wakala wa Serikali zilizo chini ya Wizara.

### Jeshi la Polisi

49. Majukumu ya Jeshi la Polisi yametajwa katika Kifungu cha 5 cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi wasaidizi Cap.322 (R.E. 2002). Jeshi la Polisi lina majukumu yafuatayo:-

(i) Kuzuia na kupambana na vitendo vya uhalifu.

(ii) Kuandaa na kufanya mapitio ya sera na sheria zinazohusiana na ulinzi na usalama wa raia.

(iii) Kuanzisha programu za muda mfupi na mrefu za kudhibiti uhalifu nchini.

(iv) Kushirikiana na jamii kuanzisha mikakati ya kuzuia na kushughulikia

uhalifu.

(v) Kusimamia shughuli zote zinazohusiana na ulinzi na usalama wa raia nchini.

(vi) Kuwaendeleza kitaaluma maafisa Polisi.

## Jeshi la Magereza

50. Majukumu ya Jeshi la Magereza ni kama ifuatavyo :-

(i) Kuwahifadhi wafungwa wa aina zote wanaowekwa chini ya ulinzi halali kisheria ndani ya magereza.

(ii) Kuandaa na kutekeleza programu za urekebishaji wa wahalifu na kuwafundisha wahalifu shughuli za uzalishaji na ujuzi mbalimbali kwa njia ya vitendo na ushauri.

(iii) Kuendesha shughuli na huduma za watuhumiwa (mahabusu kwa mujibu wa sheria).

(iv) Kuchangia ushauri kuhusu uzuiaji na udhibiti wa uhalifu na urekebishaji wa wahalifu

## Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

51. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lina majukumu yafuatayo:-

(i) Kuandaa Sera ya zimamoto na uokoaji.

(ii) Kusimamia shughuli zote za kuzima moto.

(iii) Kufanya shughuli za uokozi wakati wa majanga.

## Idara ya Uhamiaji

52. Idara ya Uhamiaji ina majukumu yafuatayo:-

(i) Kudhibiti uingiaji na utokaji wa watu nchini.

(ii) Kusimamia ukaazi wa wageni nchini kwa mujibu wa sheria.

(iii) Kutoa pasi za kusafiria na hati nyingine za safari kwa raia wenye sifa.

(iv) Kuratibu mchakato wa maombi ya uraia wa Tanzania kwa wageni wanaoishi nchini.

## Idara ya Wakimbizi

53. Idara ya Wakimbizi ina majukumu yafuatayo:-

(i) Kusajili waomba hifadhi na wakimbizi.

(ii) Kuratibu taratibu za kiutawala zinazotumika katika kumtambua mkimbizi iwapo anastahili kupewa hifadhi ya ukimbizi nchini.

(iii) Kusimamia mashirika ya misaada yanayofanya kazi makambini ili kuhakikisha kuwa yanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Mikataba iliyosainiwa nao kwa madhumuni hayo.

(iv) Kutoa mapendekezo kwa wafadhili juu ya misaada inayohitajika kwa ajili ya wakimbizi na maeneo yaliyoathirika na uwepo wa idadi kubwa ya wakimbizi.

(v) Kushiriki katika jitihada za Kimataifa za kupata suluhisho la kudumu la tatizo la wakimbizi.

(vi) Kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, na Mikataba mbali mbali ya Kimataifa kuhusu hifadhi ya ukimbizi nchini.

(vii) Kusimamia urejeaji wa wakimbizi kwao na kuwapokea na kuwaunganisha wakimbizi (raia wa Tanzania) wanaorejea nchini na familia zao.

**Idara ya Huduma kwa Jamii**

54. Idara ya Huduma kwa Jamii ina majukumu yafuatayo:-

(i) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Huduma kwa Jamii.

(ii) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Majaribio *"The Probation of Offenders Act,"* [Cap. 247 R.E. 2002] ambayo awali ilikuwa inasimamiwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

(iii) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Bodi za Parole Na. 25/1994 na Utaratibu wa Kifungo cha Nje *(Extra Mural Penal Employment, S. 72 of Prison Act, Na. 34/1967)* jukumu ambalo awali lilikuwa chini ya Jeshi la Magereza.

(iv) Mchakato wa kusimamia wafungwa wa kifungo cha nje (EML) na wale wanaoachiwa chini ya utaratibu wa Parole uko katika hatua za makabidhiano kati ya Jeshi la Magereza na Idara ya Huduma kwa Jamii.

**Idara ya Kushughulikia Malalamiko**

55. Idara hii imepewa majukumu yafuatayo:-

(i) Kupokea na kushughulikia malalamiko ya wananchi na wadau wengine yanayohusu Idara za utendaji zilizoko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

(ii) Kufanya ukaguzi na mahojiano kuhusu malalamiko ya wananchi.

(iii) Kupokea na kushughulikia malalamiko kutoka kwa mahabusu na wafungwa, kufanya utafiti ili kubaini chanzo cha malalamiko au sababu za utoaji duni wa huduma ndani ya Wizara, Sekta Binafsi ya ulinzi na kutoa ushauri wa njia au hatua za kuboresha utendaji.

**Idara ya Huduma za Sheria**

Majukumu ya Idara ya Huduma za Sheria ni:

(i) Kutoa ushauri wa Kisheria kwa Wizara, Idara zake na Vitengo,

(ii) Kupitisha Maombi ya Usajili wa Vyama,

(iii) Kushughulikia mashauri yote yanayohusiana na Vyama vya Kijamii.

**Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa**

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ina majukumu yafuatayo:-

(i) Kutambua uraia wa watu wanaoishi nchini na kuandikisha taarifa zao ambazo zinatambulika kitaifa na kimataifa,

(ii) Kutoa vitambulisho kwa raia na wageni wenye umri wa miaka 18 na kuendelea,

(iii) Kujenga utawala bora wa Mamlaka,

(iv) Kutunza Daftari la Taifa la Utambuzi na Usajili wa Watu.

## HALI YA UONGOZI KUANZIA 1961

56. Katika kipindi cha miaka 50 iliyopita Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeongozwa na Mawaziri 21. Mawaziri Wazalendo walioongoza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tangu mwaka 1961 ni:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mheshimiwa Sir George Kahama | - | 1961 |
| 2. | Mheshimiwa Oscar Kambona | - | 1962 |
| 3. | Mheshimiwa Lawi Sijaona | - | 1963-65 |
| 4. | Mheshimiwa Job Lusinde | - | 1966 |
| 5. | Mheshimiwa Saidi Maswanya | | 1967-73 |
| 6. | Mheshimiwa Omary Muhaji | - | 1973-74 |
| 7. | Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi | - | 1975-76 |
| 8. | Mheshimiwa Hassan N. Moyo | - | 1977-78 |
| 9. | Mheshimiwa Salmin A. Juma | - | 1979-80 |
| 10. | Mheshimiwa Abdalla Natepe | - | 1980-83 |
| 11. | Mheshimiwa Muhidin Kimario | - | 1983-89 |
| 12. | Mheshimiwa Nalaila Kiula | - | 1990 |
| 13. | Mheshimiwa Augustino L. Mrema | - | 1990-94 |
| 14. | Mheshimiwa Ernest Nyanda | - | 1995 |
| 15. | Mheshimiwa Ali Ameir Mohammed | - | 1995-99 |
| 16. | Mheshimiwa Muhammed S. Khatib | - | 2000-02 |
| 17. | Mheshimiwa Omar R. Mapuri | - | 2003-05 |
| 18. | Mheshimiwa John Z. Chiligati | - | 2006 |
| 19. | Mheshimiwa Joseph J. Mungai | - | 2006-08 |
| 20. | Mheshimiwa Lawrence K. Masha | - | 2008 -2010 |
| 21. | Mheshimiwa Shamsi V. Nahodha | - | 2010–hadi sasa |

58. Vile vile Wizara imeongozwa na Makatibu Wakuu 22. Makatibu Wakuu walioongoza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tangu Uhuru mwaka 1961 ni:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndugu Leonard Kambunga Bakuname | - | 1960-1963 |
| 2. | Ndugu Idd Rajabu Mwajasho | - | 1963-1965 |
| 3. | Ndugu Bernard Jacob Mkatte | - | 1965-1968 |
| 4. | Ndugu Fredrick Jonas Mchauru | - | 1968-1972 |
| 5. | Ndugu Godfrey Jacob Kileo | - | 1972-1975 |
| 6. | Ndugu Hosea Zakaria Talawa | - | 1975-1975 |
| 7. | Ndugu Julius Dustan Mganga | - | 1975-1977 |
| 8. | Ndugu Justine Matiko Mwita Matiko | - | 1977-1983 |
| 9. | Ndugu Elimsuri S. J. Malamia | - | 1983-1985 |
| 10. | Ndugu M.D. Mkumbwa | - | 1986-1987 |
| 11. | Ndugu R.M. Linjewile | - | 1987-1990 |
| 12. | Ndugu M.Y.C Lumbanga | - | 1990-1991 |
| 13. | Ndugu W.J. Mwabulambo | - | 1991-1993 |
| 14. | Ndugu S.L. Adel | - | 1993-1994 |
| 15. | Ndugu R .Mariki | - | 1994-1995 |
| 16. | Ndugu T.P. Magere | - | 1995-1998 |
| 17. | Ndugu B.S. Mchomvu | - | 1998-2003 |
| 18. | Ndugu Bakari A. Mahiza | - | 2003-2006 |
| 19. | Ndugu Salmon Odunga | - | 2006-2007 |
| 20. | Ndugu Mohamed S. Muya | - | 2007-2008 |
| 21. | Ndugu Patrick Rutabanzibwa | - | 2008-2009 |
| 22. | Ndugu Mbarak M. Abdulwakil | - | 2009- sasa |

## *Mawaziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuanzia 1961 (Picha)*



MHE GEORGE KAHAMA 1961


























MHE. ERNEST NYANDA - 1995


MHE ALI MOHAMMED -1995 - 99


MHE MOHAMMED KHATIB - 2000 - 02


MHE. OMAR MAPURI - 2003 - 05


MHE. LAWRENCE MASHA 2008 - 2010


MHE. SHAMSI V. NAHODHA 2010 HADI SASA

## MAFANIKIO YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

59. Katika kipindi cha miaka 50 iliyopita Wizara imepata mafanikio mbalimbali kama ifuatavyo:

**Sheria zilizoandaliwa:**

(i) Sheria ya Uhamiaji Na. 41 ya mwaka 1963 ambayo ilirekebishwa na kubadilishwa na Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 1972 na hatimaye Sheria ya Uhamiaji Na. 7 ya mwaka 1995 ambayo iliambatana na Sheria ya Uraia wa Tanzania Na. 6 ya mwaka 1995,

(ii) Sheria ya Magereza Na. 34 ya mwaka 1967,

(iii) Sheria ya Wakimbizi Na. 2 ya mwaka 1996 na hatimaye sheria Na. 9 ya mwaka 1998 iliyoiondoa ile ya mwaka 1996,

(iv) Sheria ya Huduma kwa Jamii Na. 6 ya mwaka 2002,

(v) Sheria ya Zimamoto na Uokoaji ya mwaka 1985 iliyoanzisha Brigedi ya Zimamoto na Uokoaji na hatimaye Sheria ya Zimamoto Na. 14 ya mwaka 2007 iliyoanzisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji,

(vi) Sheria ya Kudhibiti Biashara Haramu ya Kusafirisha Binadamu Na. ya mwaka 2008.

Aidha Wizara imefanikiwa kuandaa Sera ya Wakimbizi ya mwaka 2003 na mchakato umeanza wa kuandaa Sera za:

(i) Usalama wa Raia,

(ii) Sera ya Magereza,

(iii) Sera ya Uhamiaji,

(iv) Sera ya Moto.

**Nyaraka zilizoandaliwa:**

(i) Waraka kuhusu mapendekezo ya kuongeza umri wa kustaafu wa Askari Polisi wa Vyeo vya chini kutoka miaka 45 hadi 50 na 50 hadi 55.

(ii) Waraka kuhusu taarifa ya utekelezaji wa Mradi wa Vitambulisho vya Taifa.

(iii) Waraka kuhusu mapendekezo ya kuwajumuisha Askari Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

**Jeshi la Polisi**

60. Mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 50 iliyopita ni kuhakikisha kuwa usalama wa raia na mali zao unaimarishwa. Katika kipindi chote hicho, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Polisi imefanikiwa kuona kuwa amani na utulivu hapa nchini imedumishwa, licha ya changamoto za hapa na pale ambazo zimekuwa zikijitokeza. Kwa sasa Jeshi la Polisi linatekeleza programu ya Maboresho ya Jeshi hilo. Programu hii ya miaka 10 ina lengo la kuimarisha utendaji na kuboresha maslahi na upatikanaji wa nyumba bora za kuishi askari.

Programu hii imeshughulikia maeneo yafuatayo:-

(i) Kuhuishwa kwa Muundo wa Utumishi wa Jeshi la Polisi. Muundo wa Utumishi ndani ya Jeshi la Polisi ambao ulikuwa haujahuishwa tangu mwaka 1982 umefanyiwa marekebisho makubwa yakiwemo kupitia upya na kuhuisha posho na stahili mbalimbali za askari zikiwemo posho za nyumba kwa askari wanaoishi uraiani na kuwa na utaratibu maalum wa mishahara kwa watendaji wa Jeshi la Polisi.

(ii) Kuboresha mfumo wa ajira, mafunzo na upandishaji vyeo. Katika kipindi hiki mifumo ya ajira, mafunzo na upandishwaji vyeo imerekebishwa na kuwa wazi na tija zaidi. Kumbukumbu za watumishi zimeboreshwa. Aidha kwa upande wa mafunzo mabadiliko makubwa yamefanyika kwa upande wa mitaala kuvipa hadhi vyuo vya Polisi, hadi kuweza kusajiliwa kama *"Police Academies"*.



*Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, akikakagua Gwaride la askari waliomaliza mafunzo yao toka mojawapo ya Vyuo vya Polisi*

(iii) Kuanzishwa kwa Kituo cha Kuingizia Malipo *(Payroll Point)* Makao Makuu ya Jeshi la Polisi. Katika juhudi za kuboresha mfumo wa ulipaji mishahara na stahiki mbalimbali za askari, Jeshi la Polisi limeanzisha kituo cha maingizo ya malipo *"Payroll Point"* hatua ambayo imeondoa kero nyingi zilizokuwa zinatokana na ucheleweshaji wa marekebisho ya malipo kwa askari.

(iv) Kuanzishwa kwa Kitengo cha Malalamiko (askari kwa askari au raia kwa askari). Ili kuboresha mifumo ya uwajibikaji ndani ya Jeshi la Polisi, Kitengo cha Malalamiko kimeanzishwa ili kupokea na kushughulikia malalamiko ya askari na raia.

(v) Kuanzishwa kwa mikakati ya kuboresha Ofisi na Makazi ya Askari. Jeshi la Polisi linatekeleza mikakati ya kuboresha makazi ya watumishi wake ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba mpya, ununuzi wa nyumba, ukarabati wa nyumba za zamani na ununuzi wa viwanja kwa ajili ya askari.

(vi) Kuboreshwa kwa mfumo wa Mawasiliano na Upashanaji habari. Mifumo ya mawasiliano na upashanaji wa habari ndani na nje ya Jeshi la Polisi umeboreshwa. Katika eneo hili wananchi wamewezeshwa kutoa taarifa za uhalifu kwa njia ya tovuti, ujumbe mfupi badala ya kufika kituoni au kuonana na Polisi ana kwa ana.



*Baadhi ya nyumba za kisasa za makazi ya askari zilizojengwa Jijini Dar es Salaam*

(vii) Utaratibu wa nishani na zawadi. Jeshi la Polisi limeanzisha utaratibu wa kutambua mchango na kazi nzuri zinazofanywa na askari na wadau wengine zinazoleta sifa kwa Jeshi la Polisi. Chini ya utaratibu huu komandi zote za Polisi zinatakiwa kutambua na kutoa zawadi na vyeti kwa askari au wadau wengine wanaofanya kazi vizuri zaidi. Aidha, kutoa adhabu kwa wale wanaofanya kinyume cha hayo *(Carrot and stick system)*. Utaratibu huu umeongeza morali ya askari na kuchochea ari ya raia kulisaidia Jeshi la Polisi.

(viii) Kuboresha ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi na wadau wengine. Wigo wa ushirikiano baina ya Jeshi la Polisi na Taasisi nyingine za Serikali na zisizokuwa za Serikali na wananchi kwa ujumla umeongezeka kuanzia ngazi ya kitaifa hadi vituoni. Hii imejidhihirisha kutokana na misaada ya hali na mali inayopatikana kutoka Serikalini, wananchi na kwa wadau wengine.



*Wadau mbalimbali wamekuwa wakitoa misaada kwa Jeshi la Polisi, ikiwa ni pamoja na pikipiki kwa ajili ya kusaidia usafiri*

(ix) Kutekeleza mpango wa huduma za afya kwa watumishi na familia zao. Jeshi la Polisi likiwa ni sehemu ya jamii linakabiliwa na athari za maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI (*HIV/AIDS*). Katika kulikabili tatizo hili, Jeshi la Polisi linashirikiana na Tume ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na ugonjwa wa UKIMWI (*Tanzania Commission of AIDS-TACAIDS*), Taasisi binafsi kama *"Pharm Access International"*, *"Marie Stoppes Tanzania"* na Chuo Kikuu Kishiriki cha Tiba Muhimbili ambapo unafanyika utafiti wa chanjo dhidi ya maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU). Elimu ya kupambana na maambukizi imeendelea kutolewa ikiwa ni pamoja na kuwahudumia wale walioathirika kwa kuwapatia madawa ya kurefusha maisha ili kupunguza makali ya ugonjwa huo.



*Kazi kubwa ya Vituo vya Afya katika Jeshi la Polisi ni kutoa huduma za ushauri na kupima kama inavyoonekana katika Kituo hiki*

Kwa kutambua hali ya unyanyapaa, *"Pharm Access Foundation"* kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi imeanzisha kikundi cha wakereketwa ambao ni wake wa askari Polisi ambao sio askari. Hawa wanajulikana kama *"Police Woman Health Care Foundation"*. Kazi yao kubwa ni pamoja na kutoa elimu ya UKIMWI makambini na majumbani kuwatembelea waathirika kuwapa faraja na kuwaelekeza jinsi ya kuishi kwa matumiani. Kwa kiasi hali hii imesaidia kushusha idadi ya waathirika hata kupunguza idadi ya vifo vya mapema na kwa wale ambao walikuwa wamedhoofu sasa wanatumika kufanya kazi. Kwa sasa kila Mkoa una vituo vya ushauri na kupima *(Counselling and Testing Centre)* na huduma ya ushauri na kupima *(Voluntary Counselling and Testing)*. Aidha, kwa waathirika mipango inafanyika ili waweze kufanya kazi karibu na maeneo yenye huduma hizi ili kuwapunguzia makali ya athari za *HIV/AIDS*.

(x) Jeshi la Polisi tayari limefanikisha askari wote kuingizwa katika huduma ya Bima ya Afya ambayo wanaipata mtumishi, mke na wategemezi wane. Sambamba na hili, jitihada zinaendelea kuboresha hospitali, Zahanati na vituo vya afya vya Jeshi la Polisi nchi nzima. Lengo ni kuboresha na kujali afya za watumishi ndani ya Jeshi, ikiwa ni pamoja na raia.

(xi) Ofisi ya Rais kupitia Mfuko Maalum wa Kusaidia Jamii *(Presidential Trust Fund)* umekuwa ukitoa mikopo yenye riba nafuu kwa familia za Askari hususan akina Mama kwa lengo la kuanzisha biashara ndogo ndogo ili kujiongezea kipato na kujikwamua na kero za kiuchumi ikiwemo kusomesha watoto wao, kununua viwanja, kuanza ujenzi wa nyumba za kuishi pia kumudu maisha yao ya kila siku. Jumla ya Wanawake 237 katika Mikoa ya Dodoma, Ruvuma na Mwanza wamepatiwa mikopo hiyo.

(xii) Kutoa Elimu kwa Umma na ndani ya Jeshi la Polisi kuhusu UKIMWI, Kutoa ushauri kwa Wahanga wa matatizo na unyanyasaji wa kijinsia yaani *"Gender Based Violence"*.

(xiii) Kuanzishwa na kuzinduliwa kwa Madawati ya Jinsia na Watoto katika Vituo vya Polisi. Mnamo tarehe 30/04/2009 Dawati la Jinsia na Watoto lilizinduliwa rasmi katika Kituo cha Polisi Oysterbay kwa niaba ya Vituo vyote vya Polisi Tanzania. Mafanikio haya yalikwenda sanjari na kuanzishwa kwa Vituo vya Wahanga wa matukio ya unyanyasaji na Ukatili wa Kijinsia. Hadi sasa kuna Vituo 6 vya mfano Jijini Dar es Salaam (Kawe, Mzimuni, Buguruni, Ukonga, Mbagala na Kigamboni). Vituo hivyo hufanya kazi kwa kuwashirikisha watendaji wa Kata, Mabaraza ya Usuluhishi, Wakuu wa Serikali za Mitaa, Askari Kata na Dawati.

(xiv) Kuanzisha Madawati 94 ya Jinsia katika Mikoa ya Morogoro, Tanga, Pwani na Dar es Salaam mwaka 2010. Chini ya udhamini wa "WLAC", *"Tanzania Police Force – Net"* ilitoa Mafunzo ya *"Gender Based Violence"* kwa Askari wa Kanda Maalum D'Salaam wapatao 260 kutoka Vituo 18 vya Polisi. Pia ilitoa Elimu kwa Umma kuhusu dhana ya Ukatili na Unyanyasaji wa kijinsia, Sheria na adhabu stahili kwa wakosaji kupitia vyombo vya habari kama radio, kutoa Elimu kwa Umma kupitia maadhimisho ya Kitaifa/ Kimataifa kama vile Sikukuu ya Saba Saba, Nane Nane na siku 16 za Kupinga ukatili wa Kijinsia Duniani, kuandaa vipeperushi, vitabu, mabango na mitaala ya kufundishia katika Vyuo vyetu vya Polisi. Zoezi hili lilifanyika chini ya udhamini wa Serikali ya Umoja wa Nchi za Ulaya (EU).

(xv) Kushirikiana kwa mafanikio na Mashirikiano na umoja wa Polisi za Kimataifa na kikanda kama vile *"International Police Organisation"* (INTERPOL), *Southern African Regional Police Chiefs Cooperation Organisation"* (SARPCCO), *"United Nations Police"* (UNPOL), *"Eastern African Police Chiefs Cooperation Organisation"* (EAPCCO).

bomba, umeme na upakaji rangi. Aidha, karakana imeanza kujengwa katika Gereza la Wami Vijana, Morogoro kwa ajili ya kuwafundisha stadi za ufundi wafungwa vijana wa umri wa miaka 18 – 21.

(viii) Kutokana na fursa zinazotolewa Magerezani, wafungwa wawili wamefanikiwa kusoma na kuhitimu Shahada ya Kwanza ya Sheria *(LLB)* ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania wakiwa wanatumikia kifungo Gereza Kuu Ukonga, tarehe 30 Oktoba, 2007 na 1 Desemba, 2009. Mmoja kati yao hivi sasa anaendelea na masomo ya Shahada ya Uzamili katika fani hiyo *(LLM)*.

(ix) Jeshi la Magereza lina Shirika lililoanzishwa chini ya Sheria Na. 23 ya Mwaka 1974 *(The Corporation Sole Act, 1974)*. Majukumu yake ni kuzalisha na kufanya biashara kwa bidhaa zote kwenye miradi ya Kilimo, Mifugo na Viwanda Vidogo Vidogo. Shirika lina miradi 23, miradi 8 ni ya Viwanda na 15 ni ya Kilimo na Ufugaji. Katika miradi hii wafungwa hushirikishwa kupata mazoezi ya fani walizojifunza. Shirika linajiendesha kwa kutumia fedha zake katika uzalishaji *(Revolving Fund)*, isipokuwa maeneo ya uwekezaji mkubwa ambapo Serikali hununua mitambo na mashine. Shirika linatumia Kikosi cha Ujenzi cha Jeshi la Magereza kuchukua Kandarasi za Ujenzi na pia kufanya ukarabati wa miundombinu ya Magereza.

Jeshi la Magereza pia limetekeleza miradi kama ifuatavyo:-

1. Ujenzi wa nyumba 50 za Serikali Kisasa, Dodoma.
2. Ujenzi wa Jengo la Idara ya Huduma za Wakimbizi, Dar es Salaam.
3. Ujenzi wa nyumba za Polisi, Kilwa Road, Dar es Salaam.
4. Ukarabati wa Jengo la Wizara ya Sayansi na Teknolojia, Dar es Salaam.

5. Ujenzi wa Jengo la darasa Chuo cha Ustawi wa Jamii, Dar es Salaam.

6. Utengenezaji wa samani kwa ajili ya Ofisi za Wizara ya Maliasili na Utalii, Dar es Salaam.

7. Utengenezaji wa samani kwa ajili ya Taasisi mbalimbali za Kiserikali na zisizo za Kiserikali zenye thamani ya jumla ya ya shilingi 930,051,336.42.

8. Ujenzi wa Ofisi ya Maafisa Tarafa Temeke, Kawe na Ukonga, Dar es Salaam.

9. Ujenzi wa msingi wa Jengo la Maktaba ya Chuo cha Usafirishaji, Dar es Salaam.


(x) Jeshi la Magereza linawapatia mafunzo mbalimbali watumishi wake. Jeshi limefanikisha mpango wa kuwapatia watumishi mafunzo ya kitaalam kama ifuatavyo:-

1. Mitaala ya mafunzo ya ngazi zote imeboreshwa na kuwa ya viwango vya Kimataifa.

2. Wakufunzi wamepewa mafunzo *(Training of Trainers)* ili waweze kufundisha mitaala hiyo mipya.

3. Maktaba za Vyuo zimeboreshwa kimajengo, vifaa, vitabu vya kisasa na teknolojia ikiwa ni pamoja na kuwapatia Wakutubi mafunzo.

4. Kompyuta zinatumika katika Ofisi za Mikoa, Vyuo vya Magereza na baadhi ya magereza makubwa nchini. Elimu ya Matumizi ya kompyuta inatolewa kwa watumishi Chuo cha Maafisa wa Magereza Ukonga, Dar es Salaam.



*Darasa la Mafunzo ya Kompyuta katika Chuo cha Maafisa Magereza Ukonga, Dar es Salaam lililoanzishwa kwa lengo la kuimarisha elimu ya teknolojia ya habari*

(xi) Jeshi linafanya jitihada za kuwa na wataalam wake wa kutosha wa Nyanja mbalimbali za Sayansi ya Jamii kama vile Watumishi wenye taaluma ya ustawi wa Jamii na Wanasaikolojia ili kufanikisha uendeshaji wa programu za urekebishaji wa wahalifu zinazolenga kwenye saikolojia ya kila mhalifu. Programu hizi huendeshwa kwa kuwaainisha wahalifu kulingana na maeneo ya matatizo yao kisaikolojia, kuchambua vyanzo/sababu na mazingira ya wao kutenda makosa husika na kuwapatia programu muafaka zenye mchanganyiko wa ushauri nasihi *(Socio – Psychological Counseling)*.

(xii) Jeshi la Magereza mara kadhaa limejipatia ushindi wa kwanza katika mazao ya viwanda vidogo vidogo kwenye Maonesho ya Kitaifa ya Biashara ya Saba Saba na pia katika mazao ya Kilimo na Mifugo kwenye Maonesho ya Wakulima, Nane Nane.



*Rais Jakaya Mrisho Kikwete akitoa Kikombe kwa Jeshi la Magereza baada ya kuibuka washindi katika Maonyesho ya Kilimo, Nane Nane, mjini Dodoma mwezi Agosti, 2010*

(xiii) Jeshi limekuwa likihimiza matumizi ya adhabu mbadala wa kifungo kwa kutumia njia zifuatazo:-

(m) Parole ni utaratibu unaowawezesha wafungwa wenye vifungo virefu magerezani vya kuanzia miaka minne kuachiliwa kwa masharti baada ya kutumikia theluthi moja ya vifungo vyao ili wamalizie muda wa vifungo vyao ndani ya jamii. Sheria ya Parole ilitungwa Mwaka 1994 na kufanyiwa marekebisho mwaka 2002. Hadi kufikia mwezi Novemba, 2010, jumla ya wafungwa 3,600 walikuwa wameachiliwa chini ya mpango wa Parole. Hata hivyo, yapo mapendekezo ya kupanua wigo wa sheria hiyo ili wafungwa wengi wa vifungo virefu wanufaike na utaratibu huu.

(b) Sheria ya Huduma kwa Jamii ya Mwaka 2002 *(Community Service Act, 2002)* ilianzishwa kwa lengo kuu la kuboresha Urekebishaji wa Wahalifu na wakati huo huo kupunguza msongamano magerezani kwa kuwapa adhabu ya kazi

za kijamii wahalifu wenye makosa ya vifungo visivyozidi miaka mitatu ili wajirekebishe wakiwa ndani ya jamii.

(c ) Jeshi huwasilisha mapendekezo kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kumshauri atumie madaraka aliyopewa chini ya Ibara ya 45 (i) (d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 au kifungu cha 50 cha Sheria ya Magereza ya Mwaka 1967 kutoa msamaha kwa makundi mbalimbali ya wafungwa. Kati ya mwaka 2005 hadi Aprili, 2011, jumla ya wafungwa 43,599 wamenufaika na Misamaha hii ambayo husaidia kupunguza msongamano.

(xiv) Jeshi limefanya ujenzi, ukarabati na pia ununuzi wa nyumba katika vituo vilivyo na upungufu wa nyumba. Ujenzi na ukarabati wa nyumba za Maafisa na Askari umefanyika katika baadhi ya Magereza nchini yakiwemo Magereza ya Mbinga, Iringa na Igunga. Pia nyumba 38 zimenunuliwa mkoani Tanga na Morogoro na nyumba 321 zimejengwa katika maeneo mbalimbali kwa utaratibu wa kujitolea kwa kutumia rasilimali zinazopatikana katika maeneo hayo. Kati ya hizo, 90 zimekamilika na 231 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Aidha, Jeshi la Magereza limefanya ukarabati wa Jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Magereza na lilianza kutumika rasmi tarehe 31 Desemba, 2007. Aidha ukarabati umefanyika katika Magereza yenye ulinzi mkali ya Isanga, Karanga na Butimba na unaendelea katika Magereza ya Lilungu, Uyui, Ukonga na Maweni. Pia kazi ya ujenzi na ukarabati wa mabweni ya wafungwa imefanyika katika baadhi ya Magereza ambayo ni pamoja na Magereza ya Shinyanga, Iringa, Njombe na Maswa. Mifumo ya maji safi na mifumo ya maji taka imeimarishwa katika baadhi ya Magereza yakiwemo Kasulu, Nzega, Bagamoyo na Mahabusu Tanga.

(xv) Jeshi la Magereza limewahi kutoa mafunzo kwa Maafisa Magereza toka nchi za Rwanda, Burundi, Msumbiji na Swaziland. Aidha, Jeshi limetiliana saini Makubaliano ya Ushirikiano *(Memorandum of Understanding)* na Magereza ya nchi za Swaziland, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (DRC), Malawi, Zimbabwe, Zambia, Msumbiji na Rwanda. Maafisa wa Jeshi la Magereza wawili wanafanya kazi Namibia kwa mkataba tangu mwaka 1994 hadi leo hii. Pia Maafisa wengine kumi na moja wanafanya kazi Liberia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Darfur na Sudan ya Kusini kwa mkataba kusaidia kufufua Mfumo wa Magereza chini ya mpango wa Umoja wa Mataifa wa kulinda Amani (*United Nations Peacekeeping Mission)*.

(xvi) Jeshi la Magereza limekuwa mstari wa mbele katika shughuli za michezo na kujipatia mafanikio makubwa tangu Uhuru. Katika miaka ya 1960 Jeshi lilifanya vizuri katika soka hadi kutoa zaidi ya nusu ya wachezaji wa Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu. Kutokana na umahiri huo, Timu ya Jeshi la Magereza ilifanikiwa kuwa Klabu Bingwa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1999/2000. Vivyo hivyo Timu za Mpira wa Mikono zimewahi kuwa Mabingwa wa Taifa na Afrika Mashariki na Kati mwaka 1993 kwa wanaume na ushindi wa pili kwa wanawake. Jeshi pia limetoa wanariadha mashuhuri na kuwa Bingwa wa Jamhuri ya Muungano kwa Mchezo wa Magongo (Hockey) kwa mwaka 2011.

(xvii) Jeshi la Magereza limeanzisha mfumo wa uendeshaji wa shughuli za wafungwa (*Offenders Management Information System)* katika eneo la kuanzia la Mkoa wa Dar es Salaam *(Pilot Area)* tarehe 17 Desemba, 2010 na Uendeshaji wa Shughuli za Utumishi *(Human Resources Management)* Julai, 2010.

(xviii) Tarehe 19/05/2008 Jeshi la Magereza lilianza kutekeleza jukumu la kuwasafirisha mahabusu kwenda Mahakamani na kurudi gerezani katika eneo la majaribio Mkoani Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani baada ya jukumu hilo kurejeshwa kutoka Polisi. Usafiri unaotumika ni mabasi badala ya makarandinga yaliyokuwa yanatumika awali.

(xix) Baadhi ya vituo vya Jeshi la Magereza nchini vimewezeshwa kutoa huduma za Kupima na kupata Ushauri kwa hiari *(Voluntary Counselling and Testing – VCT)* na Vituo *"Care and Treatment Centre"* (CTC) na lengo ni kwamba ifikapo 2011 mikoa yote ya Tanzania Bara iwe angalau na kituo kimoja chenye hadhi ya aina hiyo.



*Kamishna Mkuu wa Jeshi la Magereza, Augustino Nanyaro akijaribisha moja ya mabasi ya Mradi wa Kusafirisha Mahabusu yaliyotolewa na Mpango wa Maboresho ya Sekta ya Sheria*

(xx) Katika kufanikisha ustawi wa watumishi wa Jeshi la Magereza, Jeshi lilianzisha Chama cha Kuweka na Kukopa *(Tanzania Prisons Savings and Credit Cooperative Society – TPS SACCOS)* tarehe 11 Agosti, 2005 ili kuwezesha watumishi kupata mikopo kwa ajili ya maendeleo binafsi.

Hivi sasa Chama kina wanachama 9,246 na kina mtaji wa jumla ya shilingi bilioni tatu na milioni mia tano za kitanzania (3.5b). Aidha Jeshi limefanikiwa kuwaingiza Maafisa na Askari wake kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.



*Baadhi ya vifaa vya kisasa vinavyotumika katika kuzima moto na kuokoa maisha*

**Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

62. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepata mafanikio yafuatayo:-

(i) Kuongezeka kwa vitendea kazi yakiwemo magari ya kisasa ya kuzimia moto katika Viwanja vya Ndege, Bandari, Halmashauri za Jiji, Manispaa na miji ambayo yameongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za zimamoto nchini.

(ii) Idadi kubwa ya Askari wa Zimamoto wamepatiwa mafunzo ya kuzimamoto na kuokoa, ndani na nje ya nchi. Aidha, jumla ya Askari 509 wamepatiwa mafunzo ya Uaskari kupitia Chuo cha Magereza Kiwira Mbeya.

(iii) Ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto unaendelea kufanywa kwenye majengo na vyombo vya usafiri na usafirishaji na elimu ya moto inatolewa kwa jamii. Pamoja na ukaguzi huo, lengo kuu la utoaji wa elimu hiyo ni kupunguza athari za majanga ya moto kwa kujenga uelewa wa namna ya kuepukana au kuondokana na uzembe unaosababisha moto.

(iv) Kuongezeka kwa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kupitia ada za ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto.

**Idara ya Uhamiaji.**


63. Idara ya Uhamiaji imepata mafanikio yafuatayo:-

(i) Baada ya uhuru shughuli zote za uhamiaji zilifanyika katika mfumo wa "*manual*". Hivi sasa shughuli nyingi zinafanywa katika mfumo wa kompyuta. Mfano, uchukuaji na utunzaji wa kumbukumbu za wageni wanaoingia na kutoka nchini, utoaji wa Visa kwa wageni wanaoomba kuingia nchini na uchapishaji wa pasipoti zinazosomeka kwa mashine.

(ii) Katika kipindi cha miaka hamsini, Idara ya Uhamiaji imefanikiwa kuwa na jengo jipya la kisasa kwa ajili ya Ofisi ya Uhamiaji Makao Makuu, Idara ina majengo 49 ya Ofisi na nyumba kwa ajili ya makazi ya Askari katika mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Kigoma, Mwanza, Kagera, Iringa, Mbeya, Arusha, Dodoma, Mara, Rukwa, Tabora na Zanzibar.

(iii) Kwa upande wa mafunzo, Idara imeanzisha Chuo cha kutoa mafunzo ya Uhamiaji "*Tanzania Regional Immigration Training Academy*" kilichopo mjini Moshi.

(iv) Idara imefunga mitambo ya kisasa ya kutunza kumbukumbu za watu wanaoingia na kutoka nchini (*Personal Identification Secure Comparizon and Evaluation System- PISCES* na *Personal Identification and Registration System – PIRS)* katika baadhi ya vituo.



*Jengo la kisasa ambalo ndio Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji jijini Dar es Salaam*

(i) Idara imeweka mfumo maalum wa utoaji wa VISA *(Visa Administration System)*. Mfumo huu wa utoaji VISA umefungwa katika vituo vya kuingia na kutoka nchini na katika Ofisi zote za Balozi za Tanzania nje ya nchi.

(ii) Idara kwa kushirikiana na UNHCR imefanikiwa kuweka mfumo wa kisasa wa elektroniki kwa ajili ya kuchapisha na kutunza kumbukumbu za Vyeti vya Uraia wa Tajnisi *(Citizenship by Naturalization Certificates)* ikilinganishwa na vile vilivyokuwa vinatolewa hapo awali kwa mfumo wa kizamani "manual" na hivyo kuwa rahisi kughushiwa.

(iii) Kwa kuwajengea uwezo wa kiuchumi watumishi wake Idara imeanzisha Chama cha Kuweka na Kukopa (Uhamiaji SACCOS) ambacho hadi sasa kina wanachama 1100 na mtaji wa shilingi bilioni moja na laki saba.

**Idara ya Wakimbizi**

64. Idara ya Wakimbizi imepata mafanikio yafuatayo:-

(i) Hadi kufikia Desemba, 2010, wakimbizi 14,000 wamesaidiwa kuungana na familia zao na wengine kupatiwa hifadhi katika nchi ya tatu *(resettlement)*.

(ii) Wakimbizi wapatao 162,256 kutoka Burundi waliokuwa kwenye makazi ya zamani ya Mishamo, Katumba na Ulyankulu wamepatiwa uraia wa Tanzania mwaka 2010.

(iii) Wakimbizi 568, 452 walirejea kwa hiari kwenye nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).



*Idadi kubwa ya wakimbizi kama hawa walirejea kwao baada ya kuhifadhiwa kwa muda mrefu nchini Tanzania*

**Idara ya Huduma kwa Jamii**

65. Idara ya huduma kwa jamii imepata mafanikio yafuatayo:-

(i) Mpaka kufikia tarehe 27 Januari, 2011 wafungwa 2,297 walikuwa wamekwishanufaika na Programu ya Huduma kwa Jamii na 72 wamenufaika na Huduma za Ujenzi wa Tabia *(Probation Services)* katika Mikoa 12 inayotekeleza shughuli za Idara. Mikoa hiyo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Shinyanga, Tanga na Mara. Idara inaendelea kusambaza huduma zake nchi nzima kwa awamu. Huduma hizi zinaipunguzia Serikali gharama za kuwalisha wafungwa na kuajiri vibarua kwenye Taasisi za Umma.

(ii) Kwa idadi ya wafungwa 2,369 walionufaika na vifungo vya nje, Serikali imeweza kuokoa kiasi kikubwa cha fedha ambazo zingetumika kuwalisha wafungwa hao kama wangetumikia adhabu zao Magerezani. Ukichukulia kwa mfano kuwa mfungwa mmoja hutumia kiasi cha shilingi 2,180 kwa siku kwa ajili ya chakula tu, wafungwa 2,369 walionufaika na vifungo nje ya Magereza, Serikali itakuwa imeokoa kiasi cha shilingi 5,164,420 kwa siku ambapo kwa mwezi ni 154,932,600. Aidha, Taasisi na Idara za Serikali zimekuwa zikiwatumia wafungwa hao kufanya kazi bila malipo na hivyo kuokoa kiasi kikubwa cha fedha ambazo zingetumika kuajiri vibarua.

(iii) Utekelezaji wa Sheria ya Huduma kwa Jamii unaimarisha familia za wafungwa wanaotumikia adhabu zao nje ya Magereza. Wafungwa waliokuwa wakitegemewa na familia, walipata fursa ya kutekeleza adhabu zao na vile vile kufanya shughuli mbalimbali za kujipatia kipato. Baadhi ya wafungwa wameajiriwa kwa muda katika Taasisi walizokuwa wakitumikia adhabu baada ya kumaliza kifungo. Aidha, kwa wafungwa ambao

sio wazoefu wamepata fursa ya kutochanganywa na wafungwa sugu na hivyo kuepuka kujifunza tabia za wahalifu sugu. Hii imesaidia wafungwa kujutia makosa yao na hivyo kutorudia kosa *(Recidivism)*.

(iv) Watumishi 100 wameajiriwa, kupewa mafunzo na kupangiwa vituo vya kazi. Kwa muda mrefu hapa nchini hapakuwepo na kada ya Maafisa Huduma kwa Jamii ambao kazi yao ni kusimamia wafungwa wanaotumikia adhabu ndani ya jamii. Baada ya kuanzisha utaratibu wa vifungo vya nje, Serikali imeweza kutoa ajira kwa watumishi 100 ambao wamepatiwa mafunzo na kutawanywa kwenye vituo vya kazi mikoani na wilayani.

(v) Tangu kuanza kwa utekelezaji wa Sheria ya Huduma kwa Jamii na ile ya Huduma za Majaribio na Ujenzi wa Tabia hapa nchini, wananchi wengi wameonekana kuzielewa na kuziunga mkono. Hali hiyo inatokana na juhudi za Idara kuihamasisha Jamii na wadau wengine kupitia Semina za mafunzo na vyombo vya habari, vipeperushi, majarida na picha za video. Mwitikio chanya umeonekana kwa wananchi kwa kutoa taarifa kwa Maafisa Huduma kwa Jamii na vyombo vingine kama Polisi pale mfungwa anapokiuka masharti aliyopewa.

(vi) Idara imeweza kuendesha Semina za Mafunzo kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Huduma kwa Jamii *(the Community Service Act, No.6/2002)* kwa wadau hususani Mahakimu, Waendesha Mashtaka, Wakuu wa vyombo vya Ulinzi na Usalama, Wasajili wa Mahakama, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi wa Jiji, Manispaa, Halmashauri na Miji na Maafisa Huduma kwa Jamii na wananchi wa kawaida kwenye mikoa inayotekeleza kazi za Idara ya Huduma kwa Jamii.

## Idara ya Kushughulikia Malalamiko

66. Tangu Februari, 2007 Idara ilipoanzishwa rasmi hadi Januari, 2011 Idara imeshughulikia malalamiko mbalimbali kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) | Mwaka 2006/2007 | - | 172 |
| (ii) | Mwaka 2007/2008 | - | 143 |
| (iii) | Mwaka 2008/2009 | - | 104 |
| (iv) | Mwaka 2009/2010 | - | 125 |
| (v) | Mwaka 2011 | - | 67 |

## Idara ya Huduma za Sheria

67. Idara Huduma za Sheria imepata mafanikio yafuatayo:

(i) Idara imekagua shughuli za vyama vya jamii ili kuongeza hamasa ya vyama kujisajili na vilivyosajiliwa kulipa ada.

(ii) Idara imeandaa benki ya kumbukumbu *"data base"* kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za Vyama vya Kijamii.

(iii) Watumishi wameelimishwa kuhusu namna ya kutumia mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu za vyama.

(iv) Jumla ya Vyama 6016 vikiwemo 832 vya Dini vimesajiliwa.


## Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa

68. Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:-


(i) Nyaraka mbalimbali za Mamlaka zimekamilika ikiwa ni pamoja na za Muundo wa Mamlaka, Kanuni za Fedha, Kanuni za Utumishi, Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na Mpango Kazi wa Mamlaka,

(ii) Mchakato wa ajira unaendelea ambapo nafasi za watendaji zimejanzwa na Mamlaka imepata kibali cha kuajiri watumishi wengine zaidi,

(iii) Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imekamilisha taratibu na hatimaye kuiwezesha Serikali kuingia mkataba rasmi na Mshauri Elekezi mwezi Januari,2010.




*Sehemu ya mbele ya Sampuli ya Kitambulisho kitakachotolewa kwa raia wa Tanzania*




*Sehemu ya mbele ya Sampuli ya Kitambulisho kitakachotolewa kwa wageni wakazi*

(iv) Mkandarasi wa kutekeleza mradi wa kutoa Vitambulisho vya Taifa amepatikana ambaye ni IRIS – Corporation Berhad kutoka nchini Malaysia,

(v) Viwanja kwa ajili ya kujenga Ofisi za Utambuzi na Usajili wa Watu katika Wilaya zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vimepatikana.

## CHANGAMOTO ZA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

69. Changamoto zinazozikabili Idara na Vitengo vya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni pamoja na:-

### Jeshi la Polisi

70. Jeshi la Polisi limekuwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Ufinyu wa bajeti ambao umekuwa kikwazo katika utekelezaji wa mipango na kazi.

(ii) Uhaba wa vitendea kazi kama vile radio za kisasa, magari, kompyutá na vifaa vingine vya kisasa.

(iii) Usambaaji wa silaha ndogondogo zinazoingizwa nchini toka nchi jirani.

(iv) Kuibuka kwa uhalifu wa kutumia mitandao ya kompyuta, fedha haramu, wizi wa kwenye mabenki kwa kupitia mashine za kutolea pesa (*ATM*) na Kadi *(Master cards)*, usafirishaji wa madawa ya kulevya, usafirishaji haramu wa binadamu pamoja na makosa ya kughushi.

(v) Upungufu wa makazi ya askari.

(vi) Ongezeko la matukio ya wananchi kujichukulia sheria mkononi.

## Jeshi la Magereza

71. Jeshi la Magereza linakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Msongamano wa wafungwa magerezani. Hivi sasa magereza yana uwezo wa kuhifadhi wafungwa 29,552 lakini wafungwa na mahabusu walioko katika magereza ni 38,000. Tatizo hili linasababishwa na kukosekana kwa Magereza ya Mahabusu katika Wilaya 39 nchini hivyo kufanya mahabusu wa Wilaya hizo kuhifadhiwa katika Wilaya nyingine jambo ambalo linasababisha msongamano. Msongamano hukwamisha juhudi za Jeshi katika kuimarisha huduma za wafungwa magerezani.

(ii) Uchakavu wa Magereza na ukosefu wa miundombinu ya maji taka na maji safi. Mpaka sasa kati ya Magereza 126 yaliyopo, magereza 24 bado yanatumia mitondoo, na Magereza 102 yanatumia mfumo wa maji taka uliokamilika ambayo ni sawa na asilimia 80.

(iii) Ukosefu wa Ofisi za Wakuu wa Magereza wa Mikoa, jambo ambalo huathiri ufanisi na utendaji wa kazi.

(iv) Uhaba wa Waganga, Wataalam wa Maabara, Wauguzi na Vituo vya Tiba.

(v) Uhaba wa nyumba za Maafisa na askari bado ni tatizo kubwa.

(vi) Uhaba wa wataalam wa nyanja mbalimbali za urekebishaji wa wahalifu kama vile Wataalamu wa Huduma za Jamii na Wanasaikolojia jambo ambalo linadhoofisha Programu za Urekebishaji wa Wahalifu.

**Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

72. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Uhaba wa magari ya kuzimia moto

(ii) Uhaba wa madawa

(iii) Ujenzi holela katika miji jambo ambalo linasababisha magari ya zimamoto kushindwa kupita wakati yanapohitajika kwenda kuzima moto

(iv) Uhaba wa vyanzo vya maji *(Fire Hydrants)* vya kutosha katika miji kwa ajili ya magari ya kuzimia moto.

(v) Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kuboresha huduma za kuzima moto na uokoaji na kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo mbalimbali vya habari.

(vi) Uhaba wa watumishi.

**Idara ya Uhamiaji**

73. Idara inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Idara inakabiliwa na upungufu wa watumishi na hivyo kufanya mkakati wa kuwa na ofisi zake katika kila Wilaya na hata Tarafa kuwa mgumu.

(ii) Idara inakabiliwa na upungufu wa Ofisi pamoja na nyumba za askari. Ofisi nyingi za Uhamiaji zimepewa nafasi finyu katika majengo mengine ya Serikali kama Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. Ofisi nyingine zipo katika nyumba za kupanga za watu binafsi, jambo ambalo linaathiri ufanisi katika utendaji kazi.

(iii) Idara ina uhaba wa vitendea kazi hali ambayo inasababisha utekelezaji wa majukumu yake mbalimbali kuwa mgumu. Uhaba huo unahusu magari, pikipiki na boti kwa ajili ya kufanya misako na doria.

(iv) Idara inakabiliwa na wimbi kubwa la wahamiaji haramu.

**Idara ya Wakimbizi**

74. Idara ya Wakimbizi inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Kuendelea kuwepo kwa Wakimbizi nchini licha ya hali ya amani kurejea katika nchi zao za asili.

(ii) Uharibifu wa mazingira kutokana na kuendelea kuwepo wakimbizi nchini.

(iii) Wakimbizi kurejea kwao na kisha kurudi tena Tanzania bila kufahamika kutokana na ukubwa na uwazi wa mipaka ya nchi yetu.

(iv) Mwamko mdogo wa mashirika yanayohudumia wakimbizi katika kusaidia kurejesha mazingira na miundombinu ya maeneo wanayoishi wakimbizi.

**Idara ya Huduma kwa Jamii**

75. Idara inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake na kupanua huduma zake nchi nzima.

(ii) Upungufu mkubwa wa watendaji yaani Maafisa Huduma kwa Jamii kwa ajili ya kusimamia wafungwa wa vifungo vya nje.

(iii) Baadhi ya Mahakimu, hususan wa Mahakama za Mwanzo kutopendelea kutumia adhabu mbadala wa kifungo Magerezani.

(iv) Uhaba wa vitendea kazi.

**Idara ya Kushughulikia Malalamiko**

76. Idara hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Ukosefu wa Sheria ya kusimamia utendaji kazi wa Idara. Mchakato wa kuipata sheria hii unaendelea.

(ii) Uhaba wa Watumishi. Mpaka sasa Idara ina jumla ya watumishi 22 wa kada mbalimbali, ambapo ikama halisi ya Idara ni watumishi 48.

(iii) Uhaba wa Vitendea kazi. Idara inakabiliwa na uhaba wa vitendea kazi kama magari na vifaa vingine.

(iv) Ufinyu wa Bajeti. Kwa muda mrefu sasa Idara imeshindwa kupata bajeti ya kutosha kukidhi mahitaji yake mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufunguzi wa Ofisi za Kanda, kujitangaza ipasavyo na kutembelea maeneo ya matukio ya malalamiko.

**Idara ya Huduma za Sheria**

77. Idara hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Kuwepo kwa sheria mbalimbali za kusajili vyama visivyo vya kiserikali na kutokuwepo kwa mawasiliano baina ya Mamlaka zinazosimamia sheria hizo. Jambo hili husababisha migongano ndani ya Serikali na hata miongoni mwa vyama vyenyewe, mfano imetokea wakati mwingine chama kukataliwa usajili chini ya sheria nyingine. Usajili wa Vyama kufanyika chini ya Sheria mbili yaani "*Societies Act*" Sura ya 337 ya mwaka 1954 iliyofanyiwa mapitio mwaka 2002, na ile ya Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali "*NGOs Act*" ya mwaka 2002.

(ii) Ufinyu wa bajeti, ambao pamoja na mambo mengine unakwamisha zoezi la ukaguzi wa vyama.

(iii) Baadhi ya vyama vimekuwa vikifanya shughuli tofauti na malengo, kama vile za siasa kinyume cha sheria ya usajili wa vyama.

(iv) Sheria ya Vyama kuandikwa kwa Kiingereza, jambo linalosababisha baadhi wa wadau kushindwa kuielewa lugha hiyo vyema.

**Mamlaka ya Vitambulisho ya Taifa**

78. Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa inakabiliana na changamoto zifuatazo:-

(i) Uelewa mdogo wa wadau na watu wengine juu ya umuhimu wa Mfumo wa Utambuzi na Usajili wa Watu.

(ii) Mifumo mingi ya Taasisi za Umma haina uwezo wa kuwasiliana.

## MATARAJIO YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 50 IJAYO

79. Wizara imepata mafanikio makubwa katika nyanja za ulinzi na usalama licha ya kukabiliwa na changamoto nyingi. Matarajio ya Wizara katika siku zijazo ni kama yafuatayo:

(i) Kuimarisha usalama kwa kutekeleza programu ya maboresho ya Jeshi la Polisi. Katika utekelezaji wa programu hii Wizara ina lengo la kulipatia Jeshi la Polisi vifaa vya kisasa, maslahi na makazi bora.

(ii) Kupunguza msongamano wa wahalifu katika magereza.

(iii) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inayo dhamira ya kupunguza tatizo la uhamiaji haramu.


(iv) Wizara imekusudia kuboresha huduma za Zimamoto na Uokaji kwa kujenga vituo vingi zaidi vya zimamoto na kwa kuanzia itajenga vituo saba katika jiji la Dar es Salaam ili kurahisisha shughuli za kuzima moto.

(v) Kuwarudisha wakimbizi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Burundi makwao kwa lengo la kuimarisha usalama wa Tanzania. Lengo ni kuona kuwa wakimbizi wote toka nchi hizi wawe wamerudi kwao ifikapo mwishoni mwa mwaka 2013.

(vi) Kuanza kutoa Vitambulisho vya Taifa mwaka 2012.

## HITIMISHO


80. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itaendelea kuyalinda mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 50 iliyopita na kushirikiana na wadau wote kuzikabili changamoto zilizopo ili kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na amani na usalama. Wizara inatambua kuwa bila amani maendeleo hayawezi kupatikana na pasipo maendeleo hakuna amani. Kwa msingi huo Wizara itaendelea kuwahimiza wananchi washiriki katika juhudi za kuimarisha amani na usalama kwa kushirikiana na vyombo vya dola ili Taifa liweze kupata maendeleo zaidi.



Askari wa Idara ya Uhamiaji wakiwa katika gwaride



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wakiwa katika harakati zao za kazi



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Balozi Khamis Kagasheki akikagua gwaride la askari wa Jeshi la Magereza

TANZANIA POLISI USALAMA WA RAIA

JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI TANZANIA KUOKOA MAISHA NA MALI

IMMIGRATION TANZANIA Migration Security and Development

Kimepigwa Chapa na Kiwanda cha Uchapaji cha
Wizara ya Elimu Press "A"
Simu: 2110092, S.L.P. 9121,
Br. ya Magogoni, Dar es Salaam